Nipashe
Jumatatu Agosti 10, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580306
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




UKURASA 11



# Rungwe apitishwa kuwania urais CHAUMA, amwaga ahadi kibao

UKURASA 4



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo ya huduma zitolewazo na Benki ya CRDB kutoka kwa Meneja Mwandamizi wa Kilimo Biashara, Shabani Maregesi (kushoto), wakati wa kilele cha maonyesho ya Nanenane kitaifa mkoani Simiyu. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Kilimo, Japheth Hasunga (wa pili kushoto) na kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Muhimbili yapokea vifaa vya mil. 300/- kutoka Korea

UKURASA 3

# Wanawake wengi wachomoza uteuzi ubunge CHADEMA

• **Majina** yote orodha awamu ya kwanza yaanikwa... *Endelea ukurasa 2*

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Fursa kwa Wagombea! 2020




Gazeti la Nipashe linatoa fursa kwa wagombea wote wa vyama vya siasa kunadi sera zao kupitia kurasa zetu kwa gharama nafuu.

**Wasiliana nasi**
**The Guardian Limited**
**Simu: 0686 101335,**
**Barua pepe: advertise@guardian.co.tz**



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

# Ni wiki ya pilikapilika

• **Kura** za wajumbe CCM kuamuliwa hatima yake...*Uk.2*



**MICHEZO** VODACOM YAAHIDI NEEMA LIGI KUU BARA UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Wanawake wachomoza uteuzi ubunge CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), jana kilitoa orodha ya awamu ya kwanza ya majina ya wagombea ubunge 163 wa Tanzania Bara, huku wanawake 'wakichomoza' kwa wingi katika awamu hiyo ya kwanza tofauti na miaka mingine iliyopita.

Katika orodha hiyo ya awamu ya kwanza wanawake wako zaidi ya 40 waliopitishwa kugombea ubunge majimboni.

Katika orodha hiyo ya awamu ya kwanza, vigogo na wabunge waliomaliza muda wao katika bunge la 11 nao 'wamechomoza' kwa wingi tena kupeperusha bendera ya chama hicho kwenye majimbo katika uchaguzi wa Oktoba 28, mwaka huu.

Orodha hiyo ilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Bara, Benson Kigaila, katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

**WANAWAKE WALIONG`ARA**

Baadhi ya wanawake waliong`ara katika orodha hiyo ya awamu ya kwanza ni Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chama hicho (BAWACHA), Halima Mdee (Kawe), Katibu Mkuu wa BAWACHA, Grace Ndendega (Kalenga), Cessilia Pareso (Karatu) na Grace Kiwelu (Vunjo).

Wengine ni Upendo Peneza (Geita Mjini), Ester Bulaya (Bunda Mjini), Ester Matiko (Tarime Mjini), Catherine Ruge (Serengeti), Hawa Mwaifunga (Tabora Mjini) na Rhoda Kunchela (Mpanda Mjini),

Katika orodha hiyo pia yumo pia Sophia Mwakagenda (Rungwe), Devotha Minja (Morogoro Mjini), Suzan Kiwanga (Mlimba), Jesca Kishoa (Iramba Magharibi) na Kunti Yusuph (Chemba).

**VIGOGO WALIONG`ARA**

Baadhi ya vigogo wa chama hicho waliong`ara ambao pia walikuwapo katika bunge lililopita ni pamoja na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe (Hai), Godbless Lema (Arusha Mjini), John Heche (Tarime Vijijini), Paschal Haonga (Mbozi), Peter Msigwa (Iringa Mjini) na Joseph Haule (Mikumi).

Pia yupo aliyewahi kuwa Mbunge wa Nyamagana katika serikali ya awamu ya nne, Ezekiel Wenye ambaye naye jina lake limerudi kwa mara nyingine na kipindi hiki akijikita katika Jimbo la Ryorya, mkoani Mara.

**SURA MPYA**

Katika orodha hiyo ya awamu ya kwanza, sura mpya zilizojitokeza ni pamoja na aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob (Ubungo), aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa BAVICHA Taifa, Patrick Sosopi (Ismani) na aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa BAVICHA Taifa, Julius Mwita (Musoma Mjini).

**MKOSAMALI APENYA**

Pia aliyewahi kuwa Mbunge wa Muhambwe, ambaye alihamia CHADEMA hivi karibuni akitokea katika chama chake cha zamani cha NCCR-Mageuzi, Felix Mkosamali, naye jina lake limerudi akigombea katika jimbo hilo hilo.



Mgombea urais kupitia CHADEMA, Tundu Lissu, akiwasalimia wananchi waliofika ofisi za chama hicho, Kanda ya Kati zilizopo eneo la Area 'C' jijini Dodoma, baada ya kuchukua fomu ya kuomba kuwania urais Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ni wiki ya pilikapilika

**Na Salome Kitomari**

WIKI hii ni ya pilikapilika kwa vyama vya siasa nchini kukiwa na mchakato wa kupata majina ya wagombea wa majimbo, udiwani huku wagombea urais wa vyama tofauti wakichukua fomu za kugombea nafasi hiyo na kuanza safari ya kusaka wadhamini 200 kila mkoa.

Kila mgombea urais kupitia chama chake cha siasa aliyechukua fomu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), anatakiwa kuwa na wadhamini 200 kila mkoa katika mikoa 10 ya Tanzania Bara na Visiwani.

Mchakato huo ulianza kwa vyama kuwa na vikao vya ndani vya mchujo wa majina ya wagombea urais wa Zanzibar na Muungano, kwa mabaraza na kamati za vyama kupitisha majina ya wanaofaa kugombea ambao walipata baraka za mkutano mkuu.

Chama cha kwanza kuanza mchakato wa kupata wagombea urais ni CCM, ambacho kilifanya vikao vyake jijini Dodoma na kuwapitisha Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Rais Dk. John Magufuli na Makamu wake, Samia Hassan Suluhu, huku Zanzibar aliyepitishwa ni Dk. Hussein Mwinyi.

Dk. Magufuli na mgombea mwenza walichukua fomu za ugombea ofisi za NEC, Agosti 6, mwaka huu, na kuanza kutafuta wadhamini mkoani Dodoma na kuendelea mikoa mingine.

NEC ilifungua pazia kwa kutoa ratiba ya kuchukua fomu na kurejesha kwa ngazi za udiwani, ubunge na urais, ambayo ilionyesha kuwa Agosti 5 hadi 25, mwaka huu ni nafasi ya urais na uteuzi utafanyika baada ya kumalizika kwa mchakato huo.

Kwenye nafasi za ubunge na udiwani, fomu zitaanza kutolewa Agosti 12 hadi 25, mwaka huu, katika ofisi za wasimamizi wa uchaguzi kwenye makao makuu ya halmashauri na kata husika.

Mgombea urais kupitia Chama cha Wakulima (AAFP), Seif Maalim Seif, alikuwa wa kwanza kuchukua fomu akiwa ameambatana na mgombea mwenza wake, Rashid Ligania.

Mwingine ni mgombea wa Chama cha Democratic Party (DP), Philipo Fumbo, akiwa na mgombea mwenza, Zainab Juma Hamisi.

Chama cha NRA, mgombea wake ni Leopord Mahona aliyeambatana na mgombea mwenza, Hamis Ali Hassan.

Agosti 7, mwaka huu, mgombea wa Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe, alichukua fomu akiwa ameambatana na mgombea mwenza, Prof. Omary Fakiy Hamad na kuanza safari ya kusaka wadhamini.

Wagombea wengine waliochukua fomu ni wa Chama cha UPDP, Twalib Kadege, na mgombea wa Chama cha ADC, Queen Sendiga, alichukua fomu na wote walianza safari ya kutafuta wadhamini.

Pia, mgombea wa Chama cha SAU, Mtamwega Mgaywa, alichukua fomu akiwa ameambatana na mgombea mwenza, Satia Bebwa.

Agosti 8, mwaka huu, mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akiwa ameambatana na mgombea mwenza, Salum Mwalimu, walianza kusaka wadhamini mkoani Singida, nyumbani alikozaliwa Lissu.

Aliyefuata siku hiyo ni mgombea urais wa Chama cha Demokrasia Makini, Cesilia Mmanga, akiwa ameambatana na mgombea mwenza, Tabu Mussa Juma.

Wiki hii vyama vingine vitaendelea kuchukua fomu kikiwamo Chama cha Wananchi (CUF), kilichotoa ratiba ya mgombea wao, Prof. Ibrahim Lipumba, kuchukua fomu leo majira ya saa tano na kuanza safari ya kusaka wadhamini kesho mkoani Morogoro.

Chama kingine ni NCCR-Mageuzi, ambacho wiki iliyopita kiliwapitisha wagombea wake, Kulwa Maghanja na mgombea mwenza.

Jana mgombea urais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, alitambulishwa na kupokelewa visiwani Zanzibar, ikiwa ni hatua ya kuendelea uchukuaji fomu za kugombea urais katika Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Mgombea urais wa CCM Visiwani humo, Dk. Mwinyi, alishatambulishwa na kupokelewa.

**KURA ZA WAJUMBE Wa CCM KUAMULIWA**

Ndani ya chama hicho mchakato wa kura za maoni kwa ngazi ya ubunge na udiwani zimekamilika na vinasubiriwa vikao vya maamuzi kuchambua majina ya watakaopeperusha bendera ya chama hicho.

CCM, baada ya kura za maoni za wajumbe wa majimbo na kata mbalimbali nchini, vikao vya wilaya na mkoa vinaendelea kupitia na kuchuja majina ya wagombea.

Mabaraza ya Wazazi wilaya, mikoa, kamati za siasa, vikao vya Halmashauri Kuu vimemaliza vikao mbalimbali vya mjadili na kupitisha majina.

Mchakato huo umeendelea kwa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), lilipitisha na kujadili majina ya wagombea wa ubunge na uwakilishi viti maalum (kundi la Vijana), Jumamosi iliyopita.

Baraza Kuu la Wazazi lilikutana jana kwa ajili ya kupiga kura za maoni kwa wagombea ubunge na Uwakilishi Viti Maalum (kundi la Wazazi).

Kwa upande wa wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), kesho watapiga kura za maoni kwa wagombea wa ubunge na Uwakilishi Viti Maalum kuandaa majina yatakayowakilishwa CCM Taifa.

Baada ya ngazi hizo kufanikisha hatua itakayofuata ni ya Kamati Kuu ya CCM Taifa kupitia majina ya wagombea ubunge, ambayo inatarajiwa kukutana mwishoni mwa wiki.

Katika vikao hivyo baadhi ya mambo yataangaliwa katika mchujo huo ambayo ni kama wagombea walianza kampeni kabla ya wakati, alifanya mbwembwe na kwenda na misafara ya watu wakishangiliwa na rushwa kutumika kushawishi wajumbe.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na NEC, kampeni za uchaguzi zitaanza Agosti 26, hadi Oktoba 27, mwaka huu, na Uchaguzi Mkuu utafanyika Oktoba 28, mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# Agizo MV Victoria kusafirisha abiria kuanzia wiki hii

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekagua ukarabati mkubwa wa meli ya MV New Victoria Hapa Kazi tu na kuagiza mamlaka inayosimamia ihakikishe kuwa kuanzia wiki ijayo meli hiyo inaanza kazi ya kusafirisha abiria na mizigo.

Amesema ianze kazi hiyo kwa kuwa ukarabati umekamilika na sasa inaendelea kukaa tu, hali ambayo ni hasara kwa serikali.

Pia, Waziri Mkuu ametoa siku mbili kwa mamlaka inayohusika na utoaji wa kibali cha kuanza kazi kwa meli hiyo ihakikishe inatoa kibali hicho haraka na ratiba ya safari itangazwe kwa sababu Watanzania wanahamu ya kuanza kuhudumiwa na meli hiyo.

Waziri Mkuu ametoa maagizo hayo jana baada ya kukagua meli hiyo ambayo tayari imeshafanya safari ya majaribio kwa kusafirisha abiria kutoka Mwanza hadi Bukoba mkoani Kagera ambako ilirudi na abiria na mizigo.

Maeneo aliyokagua kwenye meli hiyo ni vyumba vya abiria vikiwamo vyumba maalumu kwa ajili ya huduma za mama na mtoto, chumba cha kuongozea meli, vyumba vya migahawa na chumba cha injini.

"Nimeona ukarabati mkubwa uliofanywa, nimeona injini mpya, meli imekamilika na ilishafanyiwa majaribio ya aina zote kubeba abiria na kubeba mizigo na wataalamu wamejiridhisha kuwa inauwezo wa kubeba abiria na mizigo."

Waziri Mkuu aliongeza: "Haya yote ni mawazo na mipango ya Rais John Magufuli pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2015-2020. Tumetekeleza na tunaendelea kutekeleza."

Baada ya kukagua meli hiyo Waziri Mkuu alikagua ujenzi wa chelezo pamoja na meli mpya na alieleza kuwa ameridhishwa na kazi inayoendelea kufanyika na amewataka Watanzania waendelee kuwa na imani na serikali yao.

Awali, Meneja Miradi ya Kimkakati inayotekelezwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), Luteni Kanali Vitus Mapunda, alisema miradi hiyo minne ya ukarabati mkubwa wa meli ya Mv Victoria Hapa Kazi Tu, MV Butiama Hapa Kazi Tu, ujenzi wa chelezo na ujenzi wa meli mpya inayojulikana kama MV Mwanza Hapa Kazi Tu itagharimu Sh. 152,916,249,842.

Alisema ukarabati wa meli ya MV New Victoria Hapa Kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na mizigo tano 400 umegharimu Sh. 22,712,098,200. Meli hiyo itatoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Bandari ya Mwanza Kaskazini, Kemendo na Bukoba.

"MV Butiama itakayobeba abiria 200 na mizigo tani 100 ukarabati wake umegharimu Sh. 4,897,640,000. Meli hiyo itatoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Bandari ya Mwanza Kaskazini na Nansio Ukerewe. Ukarabati wa chelezo umegharimu Sh. 36,152,511,642 na ujenzi wa meli mpya utagharimu Sh. 89,154,000,000."

# Muhimbili yapokea vifaa vya mil. 300/- kutoka Korea

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH)- Mloganzila imepokea msaada wa vifaa tiba wenye thamani ya Sh. milioni 335 kutoka kwa taasisi inayojihusisha na masuala ya afya ya Korea Kusini (KOFIH).

Mkurugenzi Mkuu wa MNH, Prof. Lawrence Museru, akipokea msaada huo mwishoni mwa wiki, alisema hospitali hiyo imekuwa na ushirikiano na taasisi hiyo tangu mwaka 2017. "Ushirikiano uliopo kwa sasa kati ya taasisi hizi mbili ni kujenga uwezo kwa Hospitali ya Mloganzila katika maeneo makuu mawili ambayo ni mafunzo na vifaa tiba. Leo hii tumekabidhiwa vifaa ikijumuisha vya kufanyia upasuaji vilivyogharimu Sh. milioni 96 na vya ufundi kwa ajili ya matengenezo ya vifaa tiba vyenye gharama ya Sh. milioni 235," alisema Prof. Museru.

Alisema vifaa hivyo vitasaidia kuongeza nguvu katika upasuaji wa masikio, pua na koo katika hospitali hiyo.

Alitaja aina ya vifaa hivyo kuwa ni vya kufanyia upasuaji wa mafindofindo na nyama za pua (Tonsillectomy and Adenoidectomy) seti sita, vifaa vya uchunguzi wa masikio, pia na koo (Basic ENT) seti mbili, vifaa vya kufanyia upasuaji wa masikio na upandikizaji wa vifaa vya usikivu masikio (Mastoideoctomy), seti nne.

Vingine ni vifaa vya upasuaji wa koo kwenye njia ya hewa (Tracheostomy), seti tatu na vifaa vingine.

Prof. Museru, alisema pia wanashirikiana kuwapatia mafunzo wataalamu wa afya katika idara mbalimbali.

"Taasisi hii pia imetusaidia kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya tumepata madaktari bingwa kutoka katika vyuo mbalimbali vya Korea Kusini na hata sasa tunao madaktari wao wanaowajengea uwezo madaktari wetu," alisema Prof. Museru.

Kwa upande wake, Naibu Mwakilishi Mkazi wa KOFIH Kim Jungyoon, alisema taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na hospitali hiyo ili kuboresha huduma za afya nchini.

"Ni heshima kuwa na nafasi hii na ushirikiano mzuri kati ya KOFIH na Hospitali ya Mloganzila tutaendelea kushirikiana katika mafunzo na vifaa tiba," alisema Kim.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza kwenye banda la benki ya NMB, katika maonyesho ya Nanenane mkoani Simiyu alipotembelea banda hilo. Katikati ni Ofisa Mkuu wa wateja wadogo na wa kati wa benki hiyo, Filbert Mponzi, na Meneja wa Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse wakisikiliza. **PICHA: MPIGAPICHA WET**

# Magufuli ateua DC mpya Ilala

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua, Ng'wilabuzu Ludigija, kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala, mkoani Dar es Salaam.

Kabla ya uteuzi huo, Ludigija alikuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, na anachukua nafasi ya Mussa Chogelo, ambaye amepangiwa kazi maalum katika Ofisi ya Rais.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu ya Chamwino, Gerson Msigwa, ilisema kufuatia uteuzi huo, Rais Magufuli amemhamisha kituo cha kazi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, mkoani Katavi, Erasto Kiwale ambaye anakwenda kuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam.

Kiwale anachukua nafasi ya Ludigija ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala.

Wakati huo huo, Rais Magufuli amemteua Catherine Mashalla kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, mkoani Katavi.

Kabla ya uteuzi huo, Mashalla alikuwa Ofisa Elimu wa Manispaa ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, na anachukua nafasi ya Kiwale ambaye amehamishwa kituo cha kazi na kuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni.

Taarifa hiyo ilisema uteuzi na uhamisho wa viongozi hao umeanza jana.



Wagombea urais wa Tanzania Bara na Visiwani wa Chama cha ACT-Wazalendo wakipokelewa jana walipowasili Zanzibar, baada ya kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa chama hicho hivi karibuni, jijini Dar es Salaam. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rungwe apitishwa kuwania urais CHAUMA, amwaga ahadi kibao

**Na Thobias Mwanakatwe**

CHAMA cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), kimempitisha Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Hashim Rungwe, kuwania urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Rungwe ambaye alikuwa mgombea pekee, alipitishwa kwa kura za ndio 197 kati ya 200 zilizopigwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa chama hicho uliofanyika jana jijini Dar es Salaam, kura tatu ziliharibika.

Aidha, wajumbe wa mkutano huo walimpitisha Ali Omar Juma kuwania urais kwa upande wa Zanzibar kwa kura 195.

Rungwe awali akiomba kura kwa wajumbe wa mkutano huo, alisema iwapo wananchi wa Tanzania watampa ridhaa ya kuongoza nchi atahakikisha anaifikisha Bahari ya Hindi katika Mkoa wa Dodoma.

Akifafanua jinsi atakavyoifikisha bahari Dodoma, alisema kutachimbwa mrefeji mkubwa kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma kama ilivyo nchi Cairo ambako kulijengwa mfereji mkubwa wa Suez Canal ambao ulijengwa kwa miaka 10 nchini Misri.

Alisema jambo jingine atakalolifanya ni kuwamwagia wananchi maji kwa kutumia helikopta, kudhibiti mrundikano wa wafungwa gerezani ambapo watakuwa hawapelekwi gerezani ovyo.

"Wafungwa wataingia gerezani kwa sababu maalum tu, biashara ya kuuza maiti itafutwa, vijana watapata ajira na mikopo nchi nzima," alisema, huku akishangiliwa na wajumbe wa mkutano huo kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Rungwe aliongeza kuwa ameamua kuwania urais ili kuwakomboa wananchi ambao alidai asilimia kubwa wanakabiliwa na hali ngumu za maisha.

MGOMBEA ZANZIBAR ANENA

Kwa upande wake mgombea urais Zanzibar, Juma alisema iwapo wananchi watampa ridhaa atahakikisha anaimarisha uchumi katika visiwa hivyo.

"Zanzibar tunakabiliwa na changamoto ya uchumi, uchumi wa visiwa vingi duniani umepiga hatua kubwa, ukiangalia Uingereza, visiwa vya Caribbean, Shelisheli vimepiga hatua kiuchumi lakini kisiwa cha Zanzibar kimekuwa duni kiuchumi," alisema.

Kuhusu vyama vya siasa kuzuiliwa kufanya mikutano, Juma alisema kwa kuwa yeye ni mwanasheria watashirikiana na wananchi kupeleka hoja mahakamani kupinga suala hili kwa sababu linakwenda kinyume na sheria za nchi.

Mambo mengine atakayofanya ni kuhakikisha kunakuwa na muungano wa shirikisho na kupunguza idadi ya majeshi Zanzibar.

PSSSF Public Service Social Security Fund

## Uhakiki wa Wastaafu na Wategemezi

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma unawatangazia kuanza zoezi la uhakiki wa Wastaafu na Wategemezi, ambao ulisitishwa 18 Machi 2020 kutokana na mlipuko wa ugongwa wa homa ya mapafu na mafua makali (Covid-19).

Wastaafu na Wategemezi hao wamegawanyika katika makundi matatu:
1. Wastaafu na Wategemezi waliosimamishiwa pensheni zao kabla ya mwezi Machi 2020 na hawajahakikiwa hadi leo.

2. Wastaafu waliotakiwa kujihakiki kuanzia mwezi Machi 2020, lakini walishindwa kujihakiki na wamekuwa wakiendelea kulipwa pensheni zao kila mwezi, kundi hili litalazimika kukamilisha uhakiki kabla ya tarehe 31 Agosti 2020.

3. Wastaafu waliohakikiwa kwa njia ya simu na walikuwa wanalipwa pensheni mwezi mmoja mmoja bila malimbikizo, kundi hili litalazimika kukamilisha uhakiki kabla ya tarehe 31 Agosti 2020.

Zoezi hili linafanyika katika ofisi zote za Mfuko na unatakiwa kufika na:
- Picha moja ya Passport Size ya hivi karibuni
- Kitambulisho cha Taifa
- Taarifa za akaunti ya benki inayopokea pensheni.

Kwa maelezo zaidi piga simu bure : - **0800 110 040**

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma

Leo. Kesho. Pamoja. 0800 110 040 www.psssf.go.tz PSSSFTZ

## Wagombea urais ACT - Wazalendo wapata mapokezi makubwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAGOMBEA wa urais kwa upande wa Tanzania Visiwani na Bara wa Chama cha ACT-Wazalendo wamepokelewa kwa kishindo ajana, mjini hapa, huku mgombea wa Bara Bernad Membe akiahidi kushughulikia kesi ya viongozi wa Jumuiya ya Mihadhara ya Kiislamu (UAMSHO).

Membe alitoa ahadi hiyo alipokuwa akizungumza katika hafla ya mapokezi na wanachama wa chama hicho baada ya matembezi ya mapokezi yaliyoanzia Bandari ya Malindi, kupitia barabara ya Darajani, Michezani, Mnazimmoja na kumalizikia ofisi za ACT-Wazalendo, Vuga.

Wagombea hao wakiwa wameambatana na mgombea mwenza, Professa Omar Fakih Hamad, walikuwa katika gari ya wazi lililopambwa kwa rangi za chama hicho ya zambarau na fulana nyeupe zilizoandikwa maandishi ya 'Shikamoo Maalim Seif' huku vyombo vya ulinzi na usalama vikiwa vimeimarisha ulinzi kila kona.

Akizungumza na wafuasi wa chama hicho, Membe alisema Zanzibar ni nchi yenye vyombo vyake vya sheria na haikuwa muafaka viongozi wa UAMSHO kukamatwa Zanzibar na baadaye kesi hiyo kuhamishiwa Tanzania Bara.

"Wananchi wakinipa ridhaa ya kuwa Rais wa Tanzania siku ya kwanza baada ya kuapishwa Uwanja wa Taifa na baadaye kusaini hati ya kiapo kwa wino mwekundu, siku inayofuata nitamwagiza Mwanasheria Mkuu wa Tanzania kuhakikisha viongozi wa UAMSHO wanarejeshwa Zanzibar ili haki yao iweze kutendeka kisheria," alisema.

Alisema akipata ridhaa ya kuchaguliwa kuwa Rais atahakikisha Zanzibar inakuwa na mamlaka kamili ya kujiamulia mambo yake, bila ya kuingiliwa na mamlaka yoyote chini ya mfumo wa Muungano wa Tanzania.

Akigusia chimbuko la kuhamia upinzani katika mkutano na waandishi wa habari hapo Vuga, Membe alisema yeye alifukuzwa CCM, tofauti na viongozi waliomtangulia ambao waliwahi kujiunga na upinzani na baadaye kurudi kwenye chama hicho.

Alisema amejiunga Chama cha ACT-Wazalendo kwa matarajio ya kudumisha demokrasia ya vyama vingi na kamwe hajatumwa na Chama Cha Mapinduzi kwenda kuvuruga vyama vya upinzani.

Kwa upande wa mgombea urais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, alisema kuna kasoro katika matayarisho ya uchaguzi mkuu, mwaka huu hasa katika mfumo wa kuwapo kwa kura ya mapema inayoruhusu vyombo vya ulinzi na usalama kupiga kura siku moja kabla ya uchaguzi mkuu.

Alisema ni jambo la kushangaza utaratibu huo unatumika upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati askari wa vyombo vya ulinzi na usalama wapo wengi Tanzania bara kuliko Zanzibar, lakini hakuna utaratibu huo. Kiongozi Mkuu wa chama hicho Zitto Kabwe, alisema ukomo wa rais kuongoza vipindi viwili kwa muda wa miaka kumi unapaswa kuheshimiwa katika misingi ya utawala bora kwa kuzingatia Katiba ya nchi.

# Bashungwa afunguka bil. 27/- za TADB kununua kahawa

**Na Mwandishi Wetu,** BARIADI

SHILINGI bilioni 27 ambazo zimetolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa vyama vinne vya ushirika katika Kanda ya Ziwa Victoria zimemfanya Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, kuishukuru benki hiyo na kuipongeza kwa kuwajali wakulima. TADB imetenga Sh. bilioni 39.6 kwa ajili ya ununuzi wa kahawa katika Kanda ya Ziwa msimu wa 2019/20. Akizungumza katika banda la benki hiyo kwenye viwanja vya Nyakabindi kwenye Maonyesho ya Wakulima na Wafugaji ya Nanenane jana, Bashungwa alisema amefurahishwa na utendaji wa benki hiyo na namna inavyojitoa kuwahudumia wakulima.

"Nimetaarifiwa na Meneja wa Kanda ya Ziwa wa TADB, Mike Granta, ambaye amemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji Japhet Justine, kwamba mpaka sasa jumla ya bilioni 27 zimetolewa kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa kahawa ya wakulima hasa mkoani Kagera. Hatua hii ni muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Kagera," alisema Waziri Bashungwa.

Alisema serikali itaendelea kuweka mipango endelevu kwenye mazao yote ya kimkakati ili kupata malighafi muhimu kwa ukuaji wa sekta ya viwanda hapa nchini.

Granta alimhakikishia waziri kuwa watahakikisha kila mkulima analipwa pesa zake kwa mujibu wa taratibu zilizopo ili kuondoa malalamiko ambayo yataharibu kabisa dhamira njema ya benki hiyo.

"Tutaufanyia kazi ushauri wa waziri wa kuhakikisha kila mkulima analipwa kulingana na utaratibu tuliojiwekea ili kuondoa malalamiko. Malalamiko yatawafanya wakulima kutokuwa na imani na benki yetu," alielezaa Granta.

# DC awataka wajawazito kutumia vituo vya afya

**Na Idda Mushi,** MVOMERO

MKUU wa Wilaya ya Mvomero, Albinus Mgonya, amewataka wajawazito na wenye watoto chini ya miaka mitano kutumia fursa ya vituo vya afya, zahanati na majengo maalumu ya kutolea huduma za kliniki kwa mama na mtoto ili kupata huduma za bure za ushauri, afya ya mwili na uzazi kwa ustawi wao na watoto wao.

Alisema hayo kwenye Shule ya Msingi Dakawa, wilayani Mvomero, wakati akizungumza na wananchi wa wilaya hiyo na kuwakumbusha waajiri kuwaruhusu kinamama watumishi wa umma kupata fursa ya kwenda kuwanyonyesha watoto wao muda unapofika ili kuepuka kukaa muda mrefu kazini.

Alisema serikali imeendelea kuweka utaratibu wa kuhakikisha wahudumu wa afya wa vijiji wanatembelea wanawake hasa wanaonyonyesha na kukabiliwa na ukatili wa kijinsia, kuwapatia ushauri nasaha ili kuondokana na changamoto hiyo inayosababisha mawazo na kushindwa kutoa maziwa ya kutosha.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji na Siku ya Lishe ya Serikali za Mitaa nchini, mkoani Morogoro na kuadhimishwa kiwilaya wilayani Mvomero, Mtaalamu wa Lishe na Chakula wa wilaya hiyo, Niyonzima Bwenge, alikiri ukatili wa kijinsia kwa wanawake wanaonyonyesha unasababisha watoto wa umri wa chini ya miaka miwili kukosa haki ya msingi ya kunyonya na kuwa na afya dhoofu.

Aliwahimiza kinamama kupata huduma mbalimbali za kiafya kwa ajili ya afya ya watoto wao ikiwamo chanjo, huduma ya uzazi na ushauri nasaha juu ya ukatili kwa kinamama kwa kuwa humfanya mama kukosa muda wa kunyonyesha mtoto ama kushindwa kutoa maziwa.

Baadhi ya wazazi wenye watoto wachanga, Rachel Kikiwa na Rose Hoza, wakakiri elimu wanayoipata kwenye vituo vya kutolea huduma ni msaada kwa malezi na makuzi ya watoto wao, na kushauri kinamama wengine kuzingatia lishe bora ikiwamo maziwa ya mama na kuzingatia makundi yote ya chakula kwa watoto wao ili kuwajenga kimwili na kiakili.

# Zimamoto waongeza magari 12 kuboresha utendaji

**Na Renatha Msungu,** SIMIYU

JESHI la Zimamoto na Uokoaji, limeongeza magari 12 yaliyotengenezwa na kiwanda cha Nyumbu ili kuboresha utendaji kazi wake hasa kwenye majanga ya moto.

Kamishna wa Utawala na Fedha wa Zimamoto, Mbaraka Semwanza, alibainisha hayo wakati maonyesho ya Nanenane kwenye viwanja vya Nyakabindi mkoani hapa.

Semwanza alisema magari hayo yatawasaidia katika kazi zao za kila siku za uokoaji katika majanga ya moto yanayotokea sehemu mbalimbali.

"Tunaendelea kufanya jitihada za kuongeza vifaa, lengo ni kufanya kazi kiufasaha pale askari na watendaji wetu wanapohitajika waweze kufika kwa haraka," alisema Kamishna Semwanza.

Semwanza alisema magari hayo yako katika Kiwanda cha Nanyumbu jijini Dodoma yakitengenezwa kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika jeshi hilo.

Kamishna huyo pia alizungumzia kifaa cha kusaidia kuvuta hewa safi pale askari wao wanapokuwa katika kazi za uokoaji hususani katika majanga ya moto, akisema kimebuniwa ili kutoa huduma iliyobora katika kuwasaidia wananchi na kuokoa mali zao.

Alisema mbali na uhaba wa vifaa vya uokoaji, kuna tatizo la ujenzi holela wa makazi katika maeneo mbalimbali nchini, akibaininisha kuwa linachangia kuzorotesha utendaji kazi pale gari la Zimamoto linapotaka kwenda eneo la tukio.

"Watu wengi wanaongea kuwa magari ya Jeshi la Zimamoto yanachelewa eneo la tukio, lakini hawajui na sisi changamoto gani tunakutana nazo ambazo ni nyingi," alisema.

Alisema jeshi hilo linatumia maonyesho hayo kutoa elimu kwa wananchi jinsi ya kujikinga na majanga ya moto pamoja kutoa elimu ya kutumia vifaa vya Zimamoto kwenye sekta ya kilimo.

"Zimamoto pia imekuwa ikitoa huduma kwa wakulima kwani kuna wakati mashamba na ya maghala ya chakula yanaungua, hivyo elimu tunayoitoa hapa itawasaidia wakulima kujikinga na majanga ya moto," alisema.



Mkurugenzi Mkuu ambaye ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCBA Bank Tanzania Limited, Margaret Karume, akizungumza na wafanyakazi wa benki hiyo mpya (hawapo pichani) kwenye hafla ya kutambulishana na wafanyakazi na viongozi jijini Dar es Salaam jana, ili kuhamasisha ufanisi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vyuo visivyolipa Bima ya Afya vyapewa siku 7

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa siku saba kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kukutana na wakuu wa vyuo vikuu ili kubaini vyuo ambavyo havijawalipia Bima ya Afya wanafunzi licha ya kulipa ada.

Hatua hiyo imetokana na malalamiko yaliyotolewa na Jumuiya ya Wanafunzi Taasisi ya Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO), ya kuwapo kwa ucheleweshaji wa vitambulisho vya Bima unaotokana na vyuo kuchelewa kufikisha fedha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Akifungua mkutano mkuu wa kwanza wa jumuiya hiyo jijini hapa, Majaliwa alimwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo, kukutana na wakuu hao ili kubaini waliochelewesha fedha hizo na ni kwa wanafunzi wangapi na hatua zipi zimechukuliwa kwa wahusika.

"Katibu Mkuu Wizara ya Elimu kashughulikie hili kujua wangapi wamelipa ada, wangapi wamepata vitambulisho vya bima na wangapi hawajapata, tatizo ni nini na nani amesababisha, mshughulikiane huko huko, wiki moja inakutosha Katibu Mkuu, hadi Agosti 16, mwaka huu nitakuwa Dodoma nipate taarifa na sababu za aliyesababisha hilo na hatua zilizochukuliwa," alisema.

Aliwataka wakuu hao kueleza mfumo wanaotumia, kigezo, wangapi wamelipa ada na sababu ya wengine kutopata vitambulisho. "Kwasasa hakuna migogoro kwenye mikopo na Bodi imetengemaa, hakuna mahali panapochelewa sasa mnataka kuchokoza tena kwenye Bima, nataka nipate taarifa hizi kabla sijaingia kwenye kampeni zangu Ruangwa, na kwa kuwa nitakuwa hapa Dodoma, Mwenyekiti wa TAHLISO kupitia Waziri wa Afya wa vyuo mkaandae taarifa ya malalamiko yote ya waliolipa fedha, lakini hawajapata vitambulisho vya bima ili serikali kuwashughulikia huko vyuo vikuu," alisema.

"Kuna wakati tunakasirisha makundi haya kwa sababu ya mtu mmoja, hatuwezi kukubaliana na hili," alisema. Alisema hadi sasa Sh. trilioni 4.3 za mikopo ya elimu ya juu zimetolewa tangu kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), na kuwataka waliokopa kurejesha kwa wakati ili kuwanufaisha wengi zaidi.

Alisema fedha hizo zimenufaisha wanafunzi 527,000, hivyo wanufaika hao wahakikishe wanarejesha mikopo hiyo ili kunufaisha wanafunzi wengi zaidi.

Awali, Mwenyekiti wa TAHLISO, Peter Niboye, alisema wanajivunia kufanya kazi kwa karibu na Bodi ya Mikopo na Mfuko wa Bima ya Afya na imechangia kutokuwapo na migomo ya wanafunzi.

Aliomba kuwapo na uwakilishi wa Jumuiya hiyo kwenye taasisi muhimu za masuala ya wanafunzi ili kurahisisha kero zao kupatiwa ufumbuzi wa haraka.

"Pia, kumekuwa na ucheleweshaji wa Bima za Afya tunakuomba Waziri Mkuu fedha hizi wanafunzi walipe moja kwa moja NHIF, kwa kuwa vyuo vimekuwa vikichelewa kuwasilisha fedha hizo na hivyo wanafunzi kuchelewa kupata bima," alisema.

Kuhusu uchaguzi mkuu, alisema jumuiya hiyo inaunga mkono mlezi wao ambaye ni mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, katika uchaguzi huo na watahakikisha anashinda kwa kishindo ili kufikia malengo ya kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa viwanda.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF sisitizeni mchakato uboreshaji viwanja sasa

**TAYARI** Shirikisho la Soka nchini (TFF) kupitia Bodi ya Ligi (TPLB), imepuliza kipenga cha kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa ni siku chache tu tangu kumalizika msimu wa 2019/20 kwa Klabu ya Simba kushuhudiwa ikiutwaa ubingwa huo kwa mara ya tatu mfululizo.

Hakika ulikuwa msimu mgumu uliotokana na ligi hiyo kama zilivyo zingine duniani, kusimama kwa takribani miezi mitatu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

Mbali na changamoto hiyo, pia tumeshuhudia ligi ngumu zaidi msimu uliomalizika wa 2019/20, kwa timu tano kutoka Ligi Kuu zikishuka daraja na mbili za Ligi Daraja la Kwanza zikipanda kwa mara ya kwanza. Singida United, Lipuli FC, Ndanda, Alliance FC na Mbao FC ni timu za Ligi Kuu zilizoshuka huku Gwambina FC ya Mwanza, Ihefu FC ya Mbrali, Mbeya zikipanda Ligi Kuu, hivyo kufanya timu zitakazoshiriki ligi hiyo msimu ujao kuwa 18 kutoka 20 za msimu uliomalizika.

Pamoja na ugumu huo wa ligi ya msimu uliopita, lakini pia tulishuhudia changamoto kubwa ya ubovu wa viwanja huku TPLB kwa nyakati tofauti ikilazimika kuvifungia baadhi hadi ilipojiridhisha usalama wake kwa afya ya wachezaji na mashabiki.

Wote tunatambuka tatizo kubwa linaloviandama viwanja vya soka nchini ni ubovu wa eneo la kuchezea 'pitch', hivyo wakati huu ligi hiyo ikitarajiwa kuanza Septemba 6, mwaka huu, hatuna budi kuikumbusha TFF na TPLB kuendelea kutoa msisitizo kwa klabu ama wamiliki kuviandaa vema viwanja vyao kabla ya ligi kuanza. Ni ukweli usiopingika kwamba, msimu ulioisha zipo timu ambazo zilishindwa kupata matokeo chanya katika baadhi ya mechi kutokana na ubovu wa viwanja, hivyo kuchangia kushika nafasi zilizopo ama zingine hadi kushuka daraja.

Lakini pia, zipo klabu ambazo ziliwakosa baadhi ya wachezaji wao muhimu wa kikosi cha kwanza kutokana na kupata majeraha yaliyosababishwa na ubovu wa viwanja, hivyo kuchangia kumaliza katika nafasi ambazo hazikutarajia.

Si hayo tu, bali tunatambua pia wapo mashabiki ambao hawavutiwi kwenda uwanjani kwa sababu tu ya ubovu wa miondombinu ya viwanja, hivyo kulazimika kufuatilia ligi hiyo kupitia televisheni na kuzikosesha klabu mapato.

Kadhalika, mashabiki wamekuwa wakikosa burudani tarajiwa kutokana na wachezaji kushindwa kuonyesha soka la kuvutia, chanzo kikiwa ni ubovu wa viwanja, huku wengine wakishindwa kuzishuhudia timu zao zikicheza nyumbani kutokana na TPLB kuhamishiwa mechi zao katika viwanja vilivyokidhi vigezo. Tunaamini ili kuweza kushuhudia soka bora, la ushindani na lakuvutia na hata kumpa bingwa halali, lazima kuwapo na miundombinu bora kuanzia eneo la kuchezea hadi majukwaani kwa mashabiki ili kuwavutia kuhudhuria viwanjani, jambo litakaloongeza mapato kwa klabu.

Hilo, likifanyika kwa ubora wa hali ya juu, ni wazi mashabiki wengi nje na ndani ya nchi watavutiwa kuifuatilia ligi yetu kwa kuhudhuria uwajani ama hata kwa luninga jambo ambalo litaongeza matangazo mengi na klabu kuzidi kunufaika kimapato. Tunatambua hakuna njia mbadala kama kweli tunataka kupiga hatua kwenye soka, ni lazima TFF, serikali na hata wadau kuwa kitu kimoja katika kuhakikisha viwanja vinaboreshwa na kuzifanya timu kupata matokeo bila kutupia lawama ubovu wa viwanja. Lakini pia tunatambua zaidi ya asilimia 90 ya viwanja vya soka nchini vinamilikiwa na chama tawala, CCM, hivyo serikali ni lazima kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha uboreswaji huo unafanyika kwa wakati kwani kwa kufanya hivyo pia vitaongeza mapato serikalini.

Tunatambua mwaka huu utagubikwa na matukio mengi katika viwanja vya soka, ikiwamo mikutano ya siasa ya uchaguzi mkuu, hivyo wamiliki hawana budi kuwa makini kwa kulinda maeneo ya kuchezea na miondombinu kwa manufaa na afya kwa soka letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Msimu mpya klabu zijiandae uwanjani na kiuchumi pia

**HAKUNA** muda wa kupoteza, kwani Septemba 6, mwaka huu tu Ligi Kuu Tanzania Bara msimu mpya wa 2020/21 unatarajiwa kuanza, timu 18 zikitarajia kuumana kutafuta bingwa mpya kwa mara nyingine.

Msimu huu timu zinazotarajia kuumana ni Simba, Yanga, Azam, Mtibwa Sugar, Kagera Sugar, Coastal Union, Polisi Tanzania, JKT Tanzania, Tanzania Prisons, Gwambina, Dodoma Mji, Mbeya City, Ihefu FC, Biashara United, Mwadui, Namungo, KMC, na Ruvu Shooting.

Ikumbukwe kuwa ligi duniani kote ilisimama Machi kutokana na ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona, hivyo kiasi cha miezi mitatu kulikuwa na mapumziko ya lazima na wachezaji kutulia majumbani.

Hili ndilo limesababisha kutokuwapo kwa muda mrefu wa mapumziko, ndiyo maana msimu mpya unaanza mapema. Na hata hivyo, umechelewa, kwani mara nyingi huanza Agosti, lakini mwezi huu ligi ndiyo ilikuwa inamazilia mechi zake. Baadhi ya klabu zimetangaza kuanza tena msimu mpya Agosti 10, zikianza kukusanya wachezaji wao kwa ajili ya maandalizi. Kwa sasa kuna pilikapilika za usajili zinazoendelea, klabu zikiendelea kusaka wachezaji ambao wanaona wanaweza kuwapatia mafanikio kwenye msimu ujao wa ligi.

Wakati wakiangalia wachezaji, lakini viongozi wa klabu, hasa zile zinazoitwa au kujiita za mikoani zinatakiwa kujiandaa si kwa kusajili wachezaji wazuri tu na wenye vipaji, lakini pia kiuchumi. Mara nyingi uchumi mbovu ndiyo unaosababisha timu nyingi zisifanye vizuri kwenye ligi, au kutotoa ushindani wa kweli.

Wachezaji hawapati posho za kutosha, wanakaa muda mrefu bila mishahara, hapo hawawezi kukupa wachezaji wachezaji wachezaji kwa asilimia 100.

Unaweza kuwa na wachezaji wazuri, lakini kama watakuwa hawatimiziwi mahitaji yao, watacheza kwa kinyongo, hivyo hawatokuwa kwenye kiwango chao cha kawaida. Msimu huu tumeona timu kama Ihefu, Gwambia FC zikipanda Ligi Kuu, mashabiki wengi wamefurahia kwa sababu ya kitu kipya tu.

Ni kwamba timu hizo zinaonekana ziko vizuri kiuchumi, hivyo wanaona pamoja na kusajili wachezaji wazuri, lakini zitaleta ushindani mkubwa kutokana na kuonekana 'hazina njaa'.

Sijajua sana Dodoma Mji, timu ambayo iko chini ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kama imejipanga sawasawa kiuchumi, au itakuwa inasubiria hisani na michango kutoka kwa wabunge, lakini nayo inatakiwa ijipange kisawasawa kwani ligi ya msimu ujao inaonekana haitokuwa lelemama. Inaonekana kabisa kuwa timu ambayo itakuwa haiko vizuri kiuchumi, basi ina asilimia kubwa kushuka. Hatutegemei Ligi Kuu msimu ujao baada ya mechi kadhaa, viongozi waanze kuomba wadhamini, wafadhili au wananchi wawasaidie. Kama ni kufadhiliwa, kusaidia au kudhaminiwa kuwe sasa na si kusubiri hadi hali iwe mbaya.

Klabu yoyote haijakatazwa kuwa na miradi yake, ya kuuza jezi, vifaa vya michezo na hata biashara yoyote ile ambayo wataona inaweza kuwapatia kipato, ikiwezekana hata mashamba wanaweza kuwa nayo.

Nakumbuka miaka ya nyuma, bendi ya muziki wa dansi ya Maquiz Du Zaire, pamoja na kupiga muziki na kuingiza pesa nyingi kwa kazi hiyo, lakini ilikuwa na mashamba makubwa maeneo ya Kimara na Sinza, huku mazao yao wakiyauza sokoni Kariakoo ambako pia walikuwa na meza yao ya biashara. Hawa walijiongeza na wakaona watafute njia nyingine ya kujiongezea kipato.

Klabu pia zinaweza kuingia mkataba hata na hoteli, masoko ya kuuza vyakula, mabasi, na makampuni mbalimbali ili wapate bidhaa zao na wao kuweka nembo za biashara zao kwenye jezi.

Ni wakati sasa wa kufanya soka letu liwe la kulipwa moja kwa moja, hivyo viongozi wa klabu endapo hawawezi kuzijenga klabu zao kiuchumi basi inabidi wajitafakari wenyewe kama wanatosha kwenye nafasi zao kwa sababu hakuna timu yoyote ile inayoweza kufanikiwa kwenye soka kwa pesa za kuungaunga.

Kwa sasa hakuna tena ule mpira wa kuchangisha wananchi pesa wala kuunda Kamati za Kusaidia Ushindi, badala yake kwa sasa klabu yenyewe inatakiwa iwe na bajeti yake ili iweze kufanya vizuri.

# Ongezeko la tembo latishia wakazi Rufiji

**Na Beatrice Shayo,** RUFIJI

KUTOKANA na kuongezeka kwa tembo, wakazi wa kijiji cha Mloka Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, wamelalamikia mazao yao kuliwa na kuhofia huenda wakapatwa na njaa.

Wananchi hao wamesema baada ya serikali kudhibiti ujangili kijijini hapo, tembo wameanza kuonekana kwa wingi ikilinganishwa na awali, na kuanza kuharibu mazao yao na wengine kuvunja mashine za kusaga unga.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi hao, Mwenyekiti wa Kitongaji cha Mkange, Ally Didunda, alisema anakabiliwa na changamoto ya tembo hao kuvamia shamba lake alilolima mahindi.

"Nilikuwa nimelima mahindi heka tatu wamenisafisha, nimevuna ekari moja na wakwe zangu ekari mbili akaambuli ekari moja," alisema.

Alisema kwa mwaka huu alitegemea kupata Sh. milioni 1.5 ambazo angezitumia kwa ajili ya kulipa ada ya mtoto wake ambaye anasoma chuo kikuu.

Aliiomba serikali kuwawekea ulinzi mkubwa hasa wakulima ili mazao yao yasiendelea kuharibiwa na wanyamapori.

Naye Mussa Hassan, alisema hasara kubwa ni tembo kufanya uharibu kwenye mashine yake ya kusaga kwa kuwa wanaivunja, hivyo kumlazimu kutengeneza upya.

Alisema ameshavamiwa na tembo kwa zaidi ya mara 12, hali ambayo inamuumiza kuendelea na biashara hiyo kwa kuwa amejikuta akipata hasara kila wakati bila kupatiwa fidia.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mloka, Ali Mbiteheni, alisema wamepakana na Pori la Akiba la Selous, hivyo wanyama wengi hufika kwenye makazi yao hasa tembo mara kwa mara na kufanya uharibifu kwenye mashamba na mashine za kusaga unga.

Alisema katika kipindi cha mwezi mmoja kuanzia Aprili hadi Mei, jumla ya wakazi 50 wa kijiji hicho wamevamiwa mashamba yao na mazao kuliwa na tembo.

"Kila siku lazima tuwaone tembo wanaingia hadi nyumba za mashine ambazo zipo katikati ya kijiji na kula pumba.

Alisema taarifa hizo wanazipeleka ngazi ya wilaya na Shirika la Hifadhi (TANAPA) wanawashirikisha kuhusiana na uharibifu wa tembo.

Alisema changamoto iliyopo kuna wakati wanatoa taarifa za kuvamiwa na tembo, lakini wanawajulisha wapo kwenye majukumu mengine, hivyo wananchi kuendelea kuathirika kutokana na wahusika kuchelewa kufika.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mloka, Chake Mkali, alisema kwa kiasi kikubwa ujangili umemalizika kwani awali walikuwa wakisifika kwa vitendo hivyo.

Alisema elimu imetolewa ya kutosha kupambana na ujangili na wale ambao wanafanya biashara hiyo ya ujangili waliuawa na wengine kukimbia kijijini hapo.

"Hapa Mloka kwa sasa watu wanaogopa ujangili, zamani ni vigumu kuona tembo katika makazi yetu ama kuharibu mazao kwa sasa tunaweza kusema tembo wameongezeka kila siku, lazima tuwaone na tunapokea malalamiko ya kuharibu mazao ya wananchi," alisema.

Alisema waliokuwa wanafanya uvuvi haramu wameajiriwa kwenye mradi wa ujenzi wa umeme zaidi ya 300 kuanzia mwaka jana, ili waweze kuendesha maisha yao.



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Sekta isiyo rasmi wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), John Mwalisu (kushoto), kuhusu shughuli za shirika hilo, alipotembelea banda la NSSF katika maonyesho ya wakulima Nanenane, mkoani Simiyu. Kulia ni Kaimu Meneja wa NSSF mkoani Simiyu, Nuhu Mmbaga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SUA yabuni umwagiliaji kwa njia ya simu

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kimebuni mfumo mpya wa umwagiliaji wa bustani na mashamba unaotumia teknolojia ya simu ya mkononi maarufu kwa jina la 'Umwagiliaji Kiganjani' ili kukuza sekta ya kilimo nchini.

Mhandisi wa Idara ya Sayansi za Uhandisi na Teknolojia, Olgen Denis, alisema hayo katika Maonyesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki, mkoani hapa na kwamba SUA imedhamiria kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo nchini.

"Chuo hiki ni cha kilimo kwa hiyo tumeamua kuleta mageuzi kwenye sekta hii ili kuongeza tija katika suala zima za uzalishaji wa mazao shambani, mfumo huu utakuwa ni chachu ya uzalishaji kwa maslahi ya taifa zima," alisema Denis.

Mhandisi Denis alisema mfumo huo utamwezesha mkulima kupata taarifa mbalimbali za shamba au bustani yake kwa njia ya simu ya mkononi.

Alisema mkulima atatumia simu ya mkononi ya aina yoyote kuwasiliana na mfumo huo utakaokuwa na kifaa maalumu kitachokuwa kikisimamia umwagiliaji na mkulima atawasiliana na kifaa kwa njia ya ujumbe.

Mhandisi Denis alisema mfumo huo utamwezesha mkulima kuwasiliana na kifaa hicho popote atakapokuwa ndani ya nchi na atapotokea taarifa sahihi za umwagiliaji inayoendelea na kuzifanyia kazi ipasavyo.

"Mfumo huu mbali na kumpa taarifa mkulima kwa kuwasiliana kwa njia ya ujumbe mfupi pia utasaidia kuokoa muda na gharama za wakulima kwenda shambani kila wakati kwani utakujulisha kinachoendelea," alisema Denis.

Alisema mfumo huo hauhitaji gharama kubwa ya uendeshaji, yeyote anaweza kuutumia na bado akaendelea kufanya mambo mengine nje ya kilimo husussani watumishi wa umma kwa kuwa kila kitu atakipata kupitia simu yake.

Aliwataka wananchi kutumia fursa ya mfamo huo kuwekeza kwenye kilimo kwa kuwa ni rahisi na unatoa nafasi kwa mtu kufanya mambo mengine nje ya shamba kwa kuwa atapata kiganjani mwake.

Nao wananchi waliopata fursa ya kuona mfumo huo wamepongeza uongozi wa chuo hicho na kuomba hamasa zaidi itolewe kwa wananchi ili waweze kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao badala ya kusubiri Nanenane pekee.

John Lowoga alisema SUA wanastahili kupongezwa, lakini alishauri teknolojia zote zisisubiri wakati wa maonyesho ya Nanenane kwa kuwa baadhi ya watu huwa hawafiki kwenye mabanda ya maonyesho.

Alisema maonyesho ya Nanenane mwaka huu yamemsaidia kujua mfumo mpya wa umwagiliaji wa kutumia simu ya mkononi na kwamba ili mfumo huo uweze kuleta tija kwa taifa, chuo kinatakiwa kuutangaza ili wananchi wengi wauelewe.

# NSSF yaboresha huduma kiganjani

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limesema kuwa limefanya maboresho ya uandikishaji na uchangiaji kwa wanachama wake, ambao kuanzia sasa utafanyika kwa wanachama wenye vitambulisho vya taifa.

Aidha, uandikishaji wa wanachama kwa muundo huo utasaidia kurahisisha huduma na kuokoa muda.

Meneja wa Sekta isiyo rasmi wa NSSF, John Mwalisu, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye Maonyesho ya Wakulima Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu.

Alisema kupitia kitambulisho cha Taifa, shirika linapata taarifa zote muhimu za mwanachama na kurahisisha usajili.

Kwa mujibu wa Mwalisu, NSSF imewarahisishia mwanachama kwa kuwa sasa wanachangia kupitia simu ya mkononi popote walipo baada ya kupewa namba ya kumbukumbu kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa malipo Serikalini (GePG).

Alisema uchangiaji kupitia simu ya mkononi umeongeza ufanisi na viwango vya kuchangia vimeongezeka, na kuondoa usumbufu wa mwanachama waliolazimika kwenda ofisi za NSSF.

Meneja huo alibainisha kuwa kiwango kinachotakiwa kuchangiwa na mwanachama wa sekta isiyo rasmi kwa mwezi ni kuanzia Sh. 20,000.

Kwa mujibu wa Mwalisu, mwanachama anaweza kuona michango yake kupitia simu ya mkononi ama kwa kupakua "Application ya NSSF Taarifa inayopatikana kwenye Google Play Store."

Mmoja wa wajasiriamali walioshiriki maonyesho hayo, Joash Omeme, alisema baada ya kupewa elimu na maofisa wa NSSF aliamua kujiunga na kupatiwa kadi ya uanachama papo hapo.

Aliwashauri wajasiriamali wenzake kujiunga na NSSF ili waweze kufaidika na mafao mbalimbali yakiwamo ya uzeeni, uzazi pamoja na mikopo ya kuinua biashara zao.

Naye, Peter Chacha, mkazi wa Mwanza, aliwashauri wajasiriamali wadogo kujiunga na NSSF kwa kuwa ni sehemu salama kwao, wakulima na wavuvi.

# Miche milioni tano mkonge kuzalishwa

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kupitia kituo chake cha Mlingano kilichopo Mkoa wa Tanga, kimeanza uzalishaji wa miche milioni tano ya zao la mkonge ili kugawa kwa wakulima, lengo likiwa kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini na kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Akizungumza katika maonyesho ya kilimo kitaifa mkoani Simiyu, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema uzalishaji wa miche hiyo umeshaanza katika kituo cha Mlingano ukiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipotembelea kituo hicho.

Alisema mkonge ambalo ni zao la kimkakati, miche yake inayozalishwa ni mbegu bora ya chotola inayoitwa 11648 ambayo inatija na ukinzani wa magonjwa yanayoshambulia zao hilo ambayo imefanyiwa utafiti na wataalamu kutoka TARI.

Alisema maamuzi ya kuzalisha miche hiyo ni kutaka kuliinua zao hilo kutoka uzalishaji wa sasa ambao unafikia tani 36,000 kufika zaidi ya tani 300,000 kwa mwaka ambazo zilikuwa zikizalishwa katika kipindi cha miaka ya 60 na kuuzwa kwenye soko la dunia.

Mkurugenzi huyo alisema uzalishaji wa miche ya mkonge kwa hatua za mwanzo umelenga kuzalisha tani 120,000 katika maeneo yanayofaa kwa kwa kilimo hicho ikiwamo Morogoro, Pwani na Manyara.

Alisema mahitaji ya mkonge katika soko la dunia ni tani 500,000, na kuwa tani 36,000 zinazozalishwa hivi sasa bado ni kidogo, hivyo serikali imeamua kuwekeza hasa kwenye uzalishaji wa mbegu bora na kuzisambaza kwa wakulima waweze kuzalisha mkonge.

Bibi Shamba wa Muungano wa vyama vinavyolima mkonge mkoani Tanga (AMCOS), Monica Mizambwa, alisema katika kipindi cha msimu wa mwaka 2019/2020 wamefanikiwa kuzalisha tani 6,590 na kuingiza shilingi bilioni 20.

Hata hivyo, alisema kuwa bado kuna changamoto ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo hicho kwa kuwa wanataka kukiendeleza kutokana na serikali kutoa mwamko wa zao hilo pamoja na uzalishaji wa mbegu bora.

# Waziri: TAKUKURU haitamvumilia mtumishi mla rushwa, ubadhirifu

**Na James Mwanamyoto,** MPWAPWA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imesema haiko tayari kuchafuliwa na mtumishi wake yeyote anayejihusisha na vitendo vya rushwa na ubadhirifu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni (mstaafu) George Mkuchika, alisema hayo wakati akimkaribisha Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alipokuwa akizindua jengo la ofisi ya TAKUKURU, Wilaya ya Mpwapwa.

Alisema taasisi hiyo imejenga taswira nzuri ya kupambana na vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa rasilimali za umma katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dk. John Magufuli ambaye amejipambanua kwa vitendo kuichukia rushwa. Alimhakikishia Makamu wa Rais kuwa, TAKUKURU haitamvumilia mtumishi yeyote atakayeshiriki vitendo vya rushwa na ubadhirifu ambavyo vinakwamisha huduma kwa wananchi na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Pia, alisema amefarijika kuona TAKUKURU imeshawachukulia hatua watumishi wote wa taasisi hiyo waliohusika na ubadhirifu wa fedha za umma wakati wa ujenzi wa baadhi ya ofisi zake ikiwamo ya Chamwino iliyozinduliwa na Rais Magufuli, Julai, 22 na kubaini ubadhirifu huo baada ya kukagua jengo hilo na kutoridhishwa na thamani ya fedha iliyotumika.

"Watumishi wote waliohusika na kubainika kujihusisha na ubadhirifu wamechukuliwa hatua stahiki za kinidhamu na kisheria na watafikishwa mahakamani hivi karibuni," Mkuchika alimthibitishia Makamu wa Rais.

Awali, akitoa maelezo kuhusu jengo la ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Mpwapwa, Mkurugenzi Mkuu, Brig Jen. John Mbungo, alisema aliunda tume huru ya uchunguzi iliyobaini ubadhirifu kwenye ujenzi wa ofisi za TAKUKURU wilaya za Chamwino na Mpwapwa na kwenye ofisi ya Intelijensia Dodoma na tayari taasisi hiyo imeshawachukulia hatua za kinidhamu na kisheria kwa waliobainika na watafikishwa mahakamani hivi karibuni.

Kufuatia hatua hiyo, Brig. Jen. Mbungo amemwomba Makamu wa Rais kumfikishia taarifa hiyo Rais Magufuli ikiwa ni sehemu ya mrejesho wa utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa alipobaini ubadhirifu huo wakati akizindua jengo la TAKUKURU Wilaya ya Chamwino.




Mtaalamu wa upishi wa kiwanda cha Bia Tanzania (TBL) tawi la Mwanza, Mark Masolwa (kushoto), akimkabidhi fulana mkazi wa Lamadi, Guke Hamis, baada ya kujibu maswali yaliyohusu unywaji wa kistaarabu, kwenye maonyesho ya Nanenane katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango aitaka PPRA kujikita kuelimisha zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amesema anatambua kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), na ameitaka kuongeza wigo wa kutoa elimu ya ununuzi wa umma kupitia vyombo vya habari.

Waziri huyo alitoa maelekezo baada ya kutembelea banda la PPRA kwenye Maonyesho ya Wakulima maarufu Nanenane, yanayofanyika kitaifa mkoani Simiyu.

Aidha, Dk. Mpango amesema kuwa anasoma ripoti za ukaguzi unaofanywa na PPRA, na ameitaka kuwa sehemu ya utatuzi wa matatizo wanayoyaibua.

"Mnafanya kazi nzuri sana, ripoti zenu nimezisoma vizuri sana na mnaniandikia vizuri. Lakini, msiishie kwenye kuibua matatizo tu, muwe pia sehemu ya kuyatatua," alisema Waziri Mpango, juzi.

Akizungumzia maagizo ya Waziri Mpango, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Sheria na Mahusiano kwa Umma, Winifrida Samba, alimshukuru Waziri kwa pongezi alizozitoa kwa mamlaka hiyo, na kuahidi kufanyia kazi maagizo yake.

Naye Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, alitembelea banda hilo, na kueleza kuwa anatambua kazi nzuri inayofanywa na mamlaka hiyo. Aliitaka kuendelea kufanya kazi nzuri na wasipunguze kasi kutokana na kusifiwa.

"Kweli kazi yenu tunaiona, mnafanya kazi nzuri. Zamani kidogo kulikuwa na changamoto, lakini kwa sasa kazi yenu tunaiona na tunaitambua kwa hilo 'we commend you' (tunawapongeza)," alisema Prof. Luoga.

Viongozi wengine waliotembelea banda la PPRA na kuwapongeza ni pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, Mkuu wa Wilaya ya Meatu, Dk. Joseph Chilongani na aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagin.

Wadau na wananchi mbalimbali walipewa elimu na kuhamasishwa kuwa sehemu ya usimamizi wa ununuzi wa umma, kwa kutoa taarifa PPRA wataona kuna dalili za uvunjifu wa sheria.

HABARI KITAIFA

# OSHA, CMA zakumbushwa usalama, afya maeneo ya kazi

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Andrew Massawe, amezitaka Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA), Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), kushirikiana kuhakikisha maeneo ya kazi kunakuwapo na usalama wa afya sambamba na kupunguza migogoro.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati akifungua kikao kazi kati ya OSHA na CMA kilichokuwa na lengo la kupunguza migogoro isiyo ya lazima sehemu za kazi.

Massawe alisema OSHA na CMA zina mahusiano yanayotegemeana, kwamba ili eneo la kazi liweze kuwa na usalama na afya nzuri kwa wafanyakazi, kunatakiwa haki, sheria, kanuni itendeke na miongozo iweze kufanyiwa kazi vizuri.

Massawe alisema sehemu ya kazi zinapokuwa hazina migogoro wafanyakazi wanafanya kazi kwa amani na hivyo uzalishaji unaongezeka.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha mwaka 2019/2020, CMA ilisuluhisha migogoro zaidi ya 10,000 ambayo ni sawa na asimilia 81, huku migogoro zaidi ya 6,000 sawa na asilimia 77 ikitolewa uamuzi.

"Nitoe wito kwa CMA kuendelea kutoa elimu zaidi kwenye maeneo ya kazi, ili wafanyakazi wapate uelewa zaidi namna wanavyofanya kazi, kwa sababu OSHA ipo maeneo mengi ya kazi, hivyo wanapokuwa huko basi CMA nanyi mkatoe elimu zaidi ili wafanyakazi waweze kujua namna mnavyofanya," alisema Massawe.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema migogoro sehemu za kazi inapotolea inapelekwa CMA.

Alisema kikao kazi hicho kilikuwa na lengo la kuhakikisha kuwa migogoro sehemu za kazi zinapungua kwa sababu inarudisha nyuma lengo la serikali katika kufikia uchumi wa viwanda.

Mwenda aliongeza kuwa muda mwingi unatumika katika kutatua migogoro na kulipa fidia, panapokuwa na uelewa wa pamoja azma ya kufikia kujenga uchumi wa viwanda inafikiwa.

Alisema watu wengi wameajiriwa kwenye sekta za uzalishaji ambako sheria zisipoangaliwa vizuri zitarudisha nyuma juhudi za serikali kufikia malengo.

Ofisa Mfawidhi wa CMA, Usekelege Mpulla, alisema mafunzo waliyoyapata yatakuwa msaada katika kazi zao, hivyo ni muhimu kwa waajiri na wafanyakazi kufahamu sheria ya OSHA.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa tatu kushoto), akitazama moja ya bidhaa zinazozalishwa wa wajasiriamali wa kampuni ya uzalishaji wa mafuta ya alizeti ya Gilitu Enterprise ambao ni wateja wa Benki ya NBC, alipotembelea banda la benki hiyo kwenye viwanja vya maonyesho ya Nanenane Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu. Wanaoshuhudia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (wa pili kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack na Meneja Bidhaa na Huduma za Kibenki wa NBC, Jonathan Bitababaje (katikati). **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mkuu aiagiza NBC kuwafikia wakulima wengi

**Na Mwandishi Wetu,** BARIADI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaagiza mawaziri wanaohusika na sekta za kilimo na fedha nchini kuhakikisha huduma za kifedha ambazo ni mahususi kwa ajili ya wakulima zinazotolewa na taasisi mbalimbali nchini ikiwamo huduma ya 'NBC Shambani' zinawafikia wadau wa kilimo na kuwaletea tija kulingana na makusudio ya kuanzishwa kwake.

Majaliwa alitoa wito huo mwishoni mwa wiki alipotembelea banda la Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwenye maonyesho ya kilimo Nanenane yanayofanyika kitaifa kwenye Uwanja wa Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu.

Akiwa ameongazana na viongozi mbalimbali wakiwamo mawaziri wanaohusika na kilimo, uvuvi na fedha, Majaliwa alisema kwa kiasi kikubwa amevutiwa na huduma mbalimbali za kibenki ambazo ni mahususi kwa ajili ya wadau wa kilimo ikiwamo huduma mpya ya NBC Shambani ambazo zikisimamiwa vizuri na wadau wote ikiwamo serikali zitaleta tija kubwa kwa walengwa sambamba na kuongeza uzalishaji na ukuaji wa uchumi. "Ufanisi wa huduma hizi mahususi kwa ajili ya wakulima utaleta muamko mkubwa kwao katika kufungua akaunti za kibenki, tofauti na huko nyuma ambapo walikuwa wanashindwa kufanya hivyo kwa kuwa huduma hizo zilikuwa haziwagusi moja kwa moja," alisema na kuongeza: Hivyo, pamoja na kuwapongeza benki ya NBC nawaomba mawaziri msimamie ili kuhakikisha kweli huduma kama hii NBC Shambani na nyingine huko zinawafikia wakulima kulingana na malengo ya kuanzishwa kwake."

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alimuhakikishia Waziri Mkuu kuwa tayari wizara hiyo ipo kwenye makubaliano na taasisi zote kubwa za kifedha nchini ikiwamo benki hiyo kuhakikisha wakulima wote wanakuwa na akaunti kwenye taasisi hizo ambazo hazitakuwa na makato kwa wakulima, hivyo huduma hiyo ya NBC Shambani ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati huo muhimu.

"Lakini tulikubaliana AMCOS zote wanapopokea zile 'AMCOS Fees' waruhusiwe kutoa asilimia 50 ya hizo ada kwa ajili ya matumizi yao ila asilimia 50 ibaki kwenye akaunti zao kwa ajili ya kuendelea kuzalisha faida," alifafanua.

Awali akimkaribisha Waziri Mkuu, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema mbali na huduma hiyo ya NBC Shambani, pia benki hiyo kwa kushrikiana na wadau wengine wakiwamo wa Jumuiya wa Wafanyabiashara Wanawake na Vijana (TABWA) pamoja na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) iliendesha mafunzo maalumu ya kilimo na biashara yaliyofanyika kwa muda wa siku tatu katika maonyesho hayo.

"Ni jitihada kama hizi kwenye kilimo pamoja na kuwasaidia wajasiriamali kupitia vilabu vyetu vya kibenki ndio vimetuwezesha Benki ya NBC kuteuliwa ili kuwania tuzo za ubora za Afrika katika kuwahudumia wajasiriamali ambazo zinaakisi ufanisi wa huduma za kibenki na kifedha katika bara la Afrika," alisema.

Akifafanua kuhusu huduma ya NBC Shambani. Mkuu wa kitengo cha wateja wadogo na wakati, wa benki hiyo, Raymond Urassa, alisema inalenga kuwasaidia wadau wa kilimo kutimiza malengo yao ya biashara ya kilimo ambapo inatoa fursa kwao kuwa na akaunti ya vikundi vya wakulima kama vile AMCOS na vikundi vingine pamoja na akaunti ya mkulima mmoja mmoja.

Alisema akaunti hiyo inawawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kufurahia huduma za benki hiyo bila kukatwa gharama zozote za uendeshaji kwani haina makato na zaidi mkulima atakapokuwa na akiba kiasi kinachozidi Sh. 100,000 kwenye akaunti yake atapatiwa faida kupitia riba.

Alisema akaunti hiyo inalenga wadau wote wanaojihusisha na biashara ya kilimo wakiwamo wasambazaji wa pembejeo za kilimo, wakulima na wasafirishaji wa mazao ya kilimo.

# Wenye ulemavu wakopeshwa bil. 3.8/-

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

JUMLA ya mikopo isiyokuwa na riba yenye thamani ya Sh. bilioni 3.8 imetolewa hadi kufikia Julai mwaka 2020 kwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali nchini.

Imeelezwa kuwa lengo la Serikali ni kuwainua kiuchumi ili kuwaondoa kwenye adha ya kuombaomba na kubaki kuwa na shughuli za kufanya kuwaingizia kipato.

Fedha hizo zilitokana ni mikopo ya asilimia 2 iliyokuwa ikitolewa na kila halmashauri nchini ambapo vikundi 370 vya watu wenye ulemavu vimekopeshwa.

Kaimu Mkurugenzi kitengo cha wenye ulemavu Ofisi ya Waziri Mkuu, Philbert Kawemama, alisema hayo jana wakati akifunga mafunzo ya wawezeshaji wa huduma za afya ngazi ya jamii yaliyofanyika mjini hapa, chini ya mradi wa Ulaya unaofadhiliwa na World Vision Tanzania.

Kawemama alisema serikali imedhamiria kuwasaidia watu wenye ulemavu kwa kuwawezesha kiuchumi kupitia halmashauri zao kwa mikopo ya asilimia mbili ambayo haina riba.

Alisema ni jukumu la maofisa ustawi wa jamii kwa sasa kuhakikisha wenye ulemavu wanapata mikopo hiyo isiyokuwa na riba inayotolewa kila mwaka.

"Maofisa ustawi ni jukumu lenu muwaambie wenye ulemavu mikopo ipo, waitumie, wakope na kufanya biashara, waache kukaa na kuombaomba."

Aidha, alisema serikali imeguswa zaidi na suala la kusaidia wenye ulemavu vitimwendo (baiskeli za wenye ulemavu) ambapo itahakikisha mradi huo unakuwa endelevu hata ufadhili utakapokwisha.

Naye Mratibu wa Mradi wa Ulaya, Chilala Elisei, alisema vijana 32 wameshapewa mafunzo ya kuwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii watakaoshirikiana na watendaji wa kata, mitaa na vijiji katika kuwapata wahitaji na kuwagawia vitimwendo 40 vyenye thamani ya shilingi milioni 26 vilivyotolewa kwenye kata za Magole na Ulaya wilayani Kilosa mkoani hapa.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Sharifa Mjewa, Mkazi wa Magole, aliishukuru World Vision Kwa mafunzo waliyowapa sambamba na vifaa vya wenye ulemavu, ambapo aliahidi kwenda kutekeleza aliyofundishwa bila upendeleo.

# Mfumo uhakiki mbegu, pembejeo waanza

**Na Mwandishi Wetu,**
BARIADI

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amezindua rasmi huduma maalum ya kuhakiki pembejeo inayofahamika kwa jina la 'T-hakiki'.

T-Hakiki ni mfumo wa njia ya simu ambapo unabofya *148*52# na kuingiza namba za zilizo kwenye sehemu yenye kivuli kwenye vifungashio vya mbegu au kwenye chupa za viuatilifu ili kuthibitisha uhalisia wa pembejeo. Uzinduzi wa huduma hiyo inayolenga kuwakomboa wakulima katika mapambano dhidi ya mbegu na viuatilifu feki, ulifanyika mwishoni mwa wiki ndani ya Banda la Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), kwenye Maonyesho ya Nanenane kitaifa yanayofanyika viwanja vya Nyakabindi mkoania Simiyu.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Hasunga alisema uuzaji wa pembejeo feki za kilimo umesababisha athari kubwa kijamii na kiuchumi.

"Matokeo yake yamesababisha changamoto nyingi kwa sekta ya kilimo ambayo ndiyo sekta muhimu inayochangia kuongeza tija kwenye uchumi wa Taifa, kwa maana hiyo huduma hii ni mkombozi halisi kwa wakulima wetu," alisema.

Alisema huduma hiyo imetokana na ubunifu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), kwa kushirikiana na Kampuni ya Quincewood Group Limited na wadau wa sekta ya kilimo kama vile Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) na Taasisi ya Utafiti na Udhibiti wa Viuatilifu (TPRI), ambao sasa wamekuja na suluhisho la kiteknolojia kukomesha matumizi ya pembejeo feki.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Ukanda wa Tropiki (TPRI), Dk. Margaret Mollel, alisema ubunifu huo umeenda sambamba na malengo ya Rais John Magufuli katika kuleta mapinduzi kwenye sekta ya kilimo.

Wakati Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, alisema: Huduma hii itamsaidia mkulima kufahamu matumizi sahihi ya pembejeo hizo kupitia simu ya mkononi, hakika haya ni mapinduzi bora ambayo yatazidi kumkomboa mkulima, lakini kuisaidia Serikali kukabiliana na wafanyabiashara wa pembejeo wasio waadilifu."

"T-Hakiki itaboresha sekta ya kilimo na italinda maisha ya wakulima wengi katika kuendesha shughuli za kilimo na kulinda thamani ya fedha zao," alisema.




Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Patrick Ngwediagi (kushoto) wakipiga makofi baada ya uzinduzi wa huduma maalum ya kuhakiki pembejeo inayofahamika kwa jina la 'T-hakiki'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumia tiba asili kisa umbali mrefu

**Na Lilian Lugakingira,**
MISSENYI

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Nyankere Kata ya Mabale wilayani Missenyi mkoani Kagera, wanalazimika kutumia tiba za asili wanapougua na baadhi ya wajawazito kujifungulia kwa wakunga wa jadi, kutokana na vituo vya kutolea huduma za afya kuwa mbali.

Wakizungumza na Nipashe wakati wa kupokea zahanati iliyojengwa na Shirika la World Vision katika kijiji hicho, mmoja wao, Editha Godfrey, alisema hawana uwezo wa kukodisha pikipiki au magari kufuata huduma za afya zilipo ikiwamo Kituo cha Afya Bunazi hasa wanapougua usiku, hali inayosababisha wakati mwingine watumie tiba za asili. Editha alisema zahanati yao pekee waliyoitegemea iliteketea kwa moto Aprili mwaka jana na kulishukuru shirika hilo kuwarejeshea huduma karibu ambayo itawapunguzia adha ya kutembea kati ya saa mbili mpaka tatu kufuata huduma. "Tunaomba serikali itusaidie kuleta vifaa vyote muhimu vinavyohitajika hasa kwa wajawazito wakati wa kujifungua, pia nyumba ya mganga wa zahanati yetu ikarabatiwe ili iwe na mazingira yatakayomtia moyo wa kutuhudumia," alisema.

Aliyekuwa Diwani wa Kata ya Mabale, Ibrahimu Kaisilanga, alisema ujenzi wa zahanati hiyo ni ukombozi kwa wananchi hasa kutokana na kata nzima kutokuwa na zahanati nyingine au kituo cha afya.

"Zahanati hii sisi tunaiona kama kituo cha afya maana inategemewa na wakazi zaidi ya 7,000 wa kata Mabale, tunaomba likipatikana fungu la kuboresha huduma za afya tujengewe kituo cha afya ili wananchi wapate huduma bora karibu na makazi yao," alisema. Mwakilishi wa Meneja wa World Vision Kanda ya Kagera, Atugonza Kyaruzi, alisema ujenzi huo umegharimu Sh. milioni 149.5 inayojumuisha nguvu za wananchi Sh. milioni 2.5.

"Lengo la mradi huu ni wananchi kupata huduma za afya karibu na kupunguza vifo vya kinamama na watoto, lakini na wananchi wengine," alisema.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, Dk. Hamis Abdallah, alitaka wajawazito kuacha tabia ya kujifungulia kwa wakunga wa jadi na badala yake watumie vituo vya kutolea huduma za afya, ili kuepuka vifo visivyo vya lazima vya wanawake na watoto vinavyotokea wakati wa kujifungua.

"Nimatumaini yangu sasa baada ya ujenzi wa zahanati hii, kutakuwa na mwitikio mkubwa wa wananchi kwenda kupata huduma kwenye zahanati hii, lengo kinamama na watoto wawe salama," alisema.

Dk. Abdalah alisema katika mwaka wa fedha 2019/2020 kumekuwa na tukio la kifo cha mama mmoja aliyepoteza maisha akiwa kwa mkunga wa jadi katika kata hiyo alipokwenda kwa ajili ya kujifungua, na kuwa walifanya ufuatiliaji na kuthibitisha hilo.

# Ummy apongeza wakulima kusaidiwa

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameipongeza Benki ya NMB kwa kuendelea kuwasaidia wakulima kwa changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo.

Waziri Ummy alitoa pongezi hizo alipotembelea banda la Benki ya NMB katika maonyesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki yanayofanyika Mkoa wa Morogoro.

Awali akimkaribisha Waziri Ummy kwenye banda la NMB, Kaimu Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Mashariki, Harold Haule Lambileki, alisema benki hiyo ipo bega kwa bega na serikali katika kusaidia sekta ya kilimo kwa ujumla.

Alisema tangu mwaka 2016 hadi sasa NMB imetoa kwa wakulima zaidi ya shilingi bilioni 800 nchi nzima ili kuwasaidia wakulima kwenye mnyororo mzima wa kuongeza thamani dhidi ya mazao yao katika maeneo mbalimbali.

Alibainisha kuwa kiwango hicho cha fedha kimejikita kuanzia mkulima anapoandaa mashamba, pembejeo, uvunaji na uhifadhi na baadaye usafirishaji wa mazao ili kupunguza baadhi ya changamoto za awali kwenye sekta hiyo.

"Maana yake ni kwamba kila mkoa na kila wilaya wakulima wamefaidika na fedha tulizozitoa hata hapa Morogoro Kanda ya Mashariki wapo waliofaidika na fedha hizi, mfano wakulima wa miwa, wakulima wa katani Tanga, wakulima wa samaki Mafia, wafugaji kuku mikoa ya Pwani nao wamefaidika na wengine wengi wamenufaika na sapoti yetu," alisema Lambileki.

Aidha, alimweleza Waziri Ummy kuwa kwa mwaka huu pia NMB imetenga zaidi ya Sh. bilioni 1.9 kwa ajili ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao nchi nzima kwa vyama vya wakulima AMCOS na pia kwa mkulima mmoja mmoja wote watafaidika kwa utaratibu ambao umewekwa na benki.

Aliwaomba washiriki na wananchi wanaofika kutembelea maonyesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki kupita katika banda la benki hiyo kwani imeandaa wataalamu wanaotoa huduma vizuri kuhakikisha wanawasaidia washiriki kulingana na mahitaji.

Benki hiyo inashiriki katika maonyesho hayo kwa kutoa huduma zote kuanzia kufungua akaunti za wateja, kuhifadhi na kutoa fedha kwa wateja na pia kutoa elimu juu ya programu mbalimbali zinazowasaidia kuinua kilimo na sekta zake.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10-BORA WA EPL MSIMU WA 2019-20 UK. 12&13



# NAFASI YA AUBAMEYANG ITAZIBIKA KWA 'MAZILIONI'

Pierre-Emerick Aubameyang akisherehekea ubingwa wa FA na wachezaji wenzake baada ya kutwaa Agosti Mosi, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

BAO alilofunga Lionel Messi wakati Barcelona ikishinda 3-1 dhidi ya Napoli kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, linamfanya sasa kufikisha timu 35 tofauti alizozifunga kwenye michuano hiyo, ikiwa ni timu mbili zaidi ya mchezaji yeyote. Cristiano Ronaldo yeye amefunga dhidi ya timu 33.



**LONDON,** England

ANAWEZA kugharimu "mazilioni ya pauni kuziba nafasi yake" na kocha Mikel Arteta anataka "kukijenga kikosi akiwa naye", lakini nahodha wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang atabakia Arsenal?

Straika huyo alifunga mabao mengine, mawili wakati wa ushindi wa kukumbukwa wa Arsenal dhidi ya Chelsea katika fainali ya FA na kupata nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Amekuwa mchezaji wa nne kufunga mabao mengi kwenye dimba la Wembley zaidi ya mara moja, akiungana na straika wa zamani wa Arsenal, Ian Wright, Bryan Robson, Ian Rush na Eric Cantona.

Mashabiki wanampenda, kocha anampenda... lakini huku akiwa amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake, mchezaji huyu wa kimataifa wa Gabon mwenye umri wa miaka 31, amewachezea mechi ya mwisho 'Washikabunduki' hao wa London?

### YEYE NI NGUZO YETU

Wakati alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu majaliwa ya mshambuliaji huyo, Arteta alisema anafikiri Aubameyang atabaki.

"Anajua nini ninachofikiria kuhusu yeye. Nataka kujenga kikosi nikiwa naye. Nafikiri anataka kubaki na karibu atasaini mkataba mpya," Arteta aliiambia BBC One.

"Nafikiri nyakati hizi zinamsaidia yeye kukubali na kuamini kwamba tupo katika njia sahihi na yeye ni sehemu yake. Anapendwa na kila mtu klabu hapa. Matumaini yangu ataendelea na sisi." Lakini Aubameyang alikuwa na aibu. Alisema hakuwa na "chochote" cha kusema kabla ya kukimbia na kwenda kunyanyua kombe.

Wakati huo huo, wachezaji wenzake, Rob Holding na Emiliano Martinez walikuwa wakimsifia nahodha wao.

"Aubameyang anaonekana kufanya mambo mazuri katika kila mchezo. Yeye ndiye shujaa wetu na amefanya hayo kwa msimu wote," alisema Holding.

"Nilimwambia yeye (Aubameyang) kabla ya mchezo, wewe unakwenda kutufanya sisi tushinde mchezo," aliongeza Martinez, ambaye alikuwa akilia kwa furaha muda wote.

### KAZI YA UBUNIFU

Katika fainali ya Kombe la FA, Aubameyang alipata penalti na kuifungia Arsenal bao la kusawazisha dakika ya 28, akifuta lile la Christian Pulisic aliloifungia Chelsea.

Lakini lilikuwa ni bao lililokamata jicho la mchezaji wa zamani wa England, Danny Murphy, akiwa mtangazaji mwenza wa BBC, kwa kumuita Aubameyang "mchezaji wa daraja la juu".

"Umaliziaji ule wa Pierre-Emerick Aubameyang hakika ulikuwa wa kiwango cha juu na kuvutia sana," alisema Murphy. "Leo tumeona namna gani ni muhimu kwa Arsenal kumbakiza. Amemalizia vizuri sana."

Mshindi wa Kombe la Ligi Kuu ya England, Chris Sutton aliongeza kwenye BBC Radio 5 Live: "Aubameyang atagharimu 'mazillioni' kuziba nafasi yake. Kwa hakika kabisa ni mazillioni. Unaweza kuona kwa nini Arsenal wanataka kumbakisha.

"Kwa uhakika ni jinamizi. Aliubetua mpira mbele ya Kurt Zouma na kumfunga kiurahisi Willy Caballero. Ni moja ya mabao matamu sana kwa hakika ni kazi ya ubunifu. Ni huzuni kwamba Wembley haina shabiki yeyote ndani yake."

Na nahodha wa zamani wa Newcastle, Alan Shearer alisema Aubameyang ni "moto".

### LINI ATAJENGEWA SANAMU YAKE?

Mashabiki walikuwa na maoni tofauti kwenye mitandano ya kijamii kuhusu Aubameyang.

Chris Lord: Aubameyang ameionyesha dunia kwa nini yeye si golikipa na mmaliziaji wa daraja la juu duniani. Mpeni mkataba mpya Auba! Mabingwa tena!

Bentemisonn: Lini watamjengea Aubameyang sanamu yake? Litakuwa jambo zuri kwa Arsenal.

BigGoonerLad: Siwezi kufikiria maisha bila yeye tafafhali, tafadhali, Aubameyang saini mkataba mpya.

Aubameyang amefunga mabao 13 kwa Arsenal kwa mwaka 2020. Mchezaji mwingine pekee ambaye ameifungia klabu yake ya Uingereza angalau mabao 13 mwaka huu ni Said Benrahma, ambaye amefunga 14 kwa klabu yake ya Brentford ya Dajara la Kwanza.

Yeye ni mchezaji wa pili wa Arsenal kufunga mara mawili kwenye fainali ya FA, baada ya Reg Lewis mwaka 1950.

Straika wa kwanza katika fainali 15 zilizopita za 15 kufunga penalti, baada ya Eden Hazard kwa Chelsea mwaka 2018.

Katika umri wake wa miaka 31, Aubameyang ni mchezaji wa pili mwenye umri mkubwa kuifungia Arsenal kwenye fainali ya FA, baada ya Robert John mwaka 1932 (akiwa na umri wa miaka 33 na siku 80).

# NYOTA 12 WALIOBEBA UEFA NA KLABU NYINGI



CRISTIANO RONALDO

**LONDON,** England

LIGI ya Mabingwa Ulaya ndiyo michuano mikubwa zaidi ya soka kwa ngazi ya klabu Ulaya na imeendelea kukua tangu ilipoboreshwa mwaka 1992. Awali ilikuwa ikijulikana kama Kombe la Ulaya na klabu zimekuwa zikipambana kutengeneza historia katika mashindano hayo.

**Tangu kuboreshwa kwa mashindano hayo, wachezaji kadhaa wakubwa wamelitwaa taji hilo mikononi mwao, huku baadhi ya majina makubwa yakishindwa kulibeba kombe hilo.**

Katika zama za Ligi ya Mabingwa, klabu kama Real Madrid, Liverpool, Manchester United na Bayern Munich zote zimekuwa zikishiriki mara kwa mara.

Ni wachezaji 12 tu ndio walioshinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiwa na klabu nyingi tofauti, huku pia kuna mchezaji mmoja tu ambaye ameshinda taji hilo na klabu tatu tofauti.

Makala haya yanakuchambulia wachezaji 12 ambao wameshinda taji hilo na klabu tofauti tangu mwaka 1992...

### #12. MARCEL DESAILLY | MARSEILLE 1993, AC MILAN 1994

Marcel Desailly ni mmoja wa walinzi bora zaidi katika kizazi chake na alifurahia mafanikio akiichezea klabu na nchi yake. Akiwa amezichezea timu kama Marseille, AC Milan, Nantes na Chelsea, mlinzi huyu wa kati ameshinda mataji mengi likiwamo la Dunia na Ulaya akiwa na Ufaransa.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Mfaransa huyo alikuwa mchezaji wa kwanza kwenye historia ya mashindano hayo kushinda taji hili misimu miwili mfululizo akianza na Marseille na baadaye AC Milan.

Desailly alistaafu soka mwaka 2006 akibakia kuwa mmoja wa walinzi bora zaidi ambao Ufaransa imewahi kuwashuhudia.

### #11. PAULO SOUSA | JUVENTUS 1996, BORUSSIA DORTMUND 1997

Paulo Sousa alikuwa na wakati mzuri mwishoni mwa miaka ya 1990, alijijengea jina yeye mwenyewe kama kiungo bora zaidi wakati akiichezea timu ya Juventus. Raia huyu wa Ureno alikuwa mmoja wa wachezaji wa 'Bianconeri' ambaye alikuwa hapewi nafasi kubwa, wakati wakiifunga Ajax mwaka 1996 na kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika kipindi hichohicho cha majira ya joto, Sousa alihamia Borussia Dortmund, ambako alitengeneza historia kwa kulibeba akiwa na miamba hao wa Bundesliga. Akaingia kwenye historia ya kuwa mmoja kati ya wachezaji wanne kushinda taji hilo misimu miwili mfululizo.

### #10. DIDIER DESCHAMPS | 1993 MARSEILLE, 1996 JUVENTUS

Mchezaji mwenzake na Marcel Desailly mwaka 1993 akiwa na Marseille na Paulo Sousa mwaka 1996 kule Juventus, Didier Deschamps alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na timu mbili tofauti.

Akiwa amezichezea klabu kadhaa zikiwamo Valencia na Chelsea, Mfaransa huyo alikuwa nguzo ya kiungo wa kati wakati akiwa Juventus.

Kwa sasa ni kocha wa timu ya Taifa ya Ufaransa na alishinda Kombe la Dunia mwaka 2018, akishinda pia akiwa mchezaji mwaka 1998.

### #9. EDWIN VAN DER SAR | AJAX 1995, MANCHESTER UNITED 2008

Anatajwa kama mmoja wa magolikipa bora zaidi katika kizazi chake, Edwin van der Sar alisubiri miaka 13 kushinda taji lake la pili la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kushinda la kwanza.

Van der Sar alikuwa shujaa wakati akiichezea Manchester United kwenye fainali dhidi ya Chelsea mwaka 2008 kwa kuokoa penalti ya Nicolas Anelka pale mjini Moscow.

### #8. CLARENCE SEEDORF | AJAX 1995, REAL MADRID 1998, AC MILAN 2003 & 2007

Clarence Seedorf ni mmoja wa viungo bora zaidi katika kizazi chake wakati akicheza kwa zaidi ya miongo miwili.

Kiungo huyo ndiye mchezaji pekee kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kushinda taji hilo akiwa na timu tatu tofauti. Hadi anastaafu kucheza soka, Mholanzi huyo amebeba taji hilo mara nne.

### #7. DECO | FC PORTO 2004, BARCELONA 2006

Huyu ni mzaliwa wa Brazil, lakini kiungo wa zamani wa Ureno ambaye alishinda kwa mara ya kwanza akiwa na kocha Jose Mourinho mwaka 2004 na FC Porto.

Akiwa na Ronaldinho katika kikosi cha kocha, Frank Rijkaard, Deco pia alikuwa mchezaji muhimu kwa Barcelona wakati wakilitwaa taji hilo mwaka 2006 kwa kuifunga Arsenal kwenye fainali.

### #6. SAMUEL ETO'O | BARCELONA 2006 & 2009, INTER MILAN 2010

Samuel Eto'o anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote wa Afrika na Cameroon. Alikuwa sehemu ya kikosi kilichoshinda mara mbili taji hilo katika Klabu ya Barcelona chini ya Pep Guardiola na Frank Rijkaard.

Pia akashinda msimu wa 2009-10 akiwa na Inter Milan chini ya kocha Jose Mourinho.

Eto'o ni mchezaji pekee katika historia ya mchezo wa soka kushinda mara mbili mfululizo mataji matatu kwa msimu katika nchini mbili tofauti, akiwa ameshinda na Barcelona na baadaye Inter Milan.

### #5. GERARD PIQUE | MANCHESTER UNITED 2008, BARCELONA 2009, 2011 & 2015

Gerard Pique alikuwa sehemu ya kikosi cha Manchester United kilichoshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2008 kabla ya kurudi Barcelona.

Chini ya kocha, Pep Guardiola, Pique alikuwa mmoja wa walinzi bora duniani akicheza kwa upatina na Carles Puyol na akabeba mara tatu taji hilo kule Barcelona.

### #4. XABI ALONSO | LIVERPOOL 2005, REAL MADRID 2014

Xabi Alonso ni mmoja wa viungo wanaoheshimika sana katika kizazi chake. Alijiunga na Liverpool kipindi cha majira ya joto mwaka na 2004 na haraka akawa mchezaji muhimu kwa kikosi cha kocha, Rafa Benitez chini ya nahodha, Steven Gerrard.

Alishinda mwaka 2005 katika fainali inayoitwa "miujiza ya Istanbul" dhidi ya AC Milan 2005 na baadaye akashinda kwa mara ya pili akiwa na Real Madrid.

### #3. DANIEL STURRIDGE | CHELSEA 2012, LIVERPOOL 2019

Daniel Sturridge aliweka historia kipindi cha majira ya joto mwaka 2019, wakati alipokuwa mchezaji wa kwanza kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na timu mbili tofauti za Ligi Kuu ya England. Alishinda mwaka 2012 akiwa na Chelsea na mwaka 2019 akiwa na Liverpool.

### #2. TONI KROOS | BAYERN MUNICH 2013, REAL MADRID 2016, 2017 & 2018

Toni Kroos ni mmoja wa viungo bora kabisa katika kizazi chake. Mjerumani huyu alifanya yake kule Bayern Munich.

Wakati Bayern Munich wanalibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2013 katika fainali dhidi ya Borussia Dortmund, yeye alikuwa mmoja wa wachezaji waliotoa mchango mkubwa.

Baadaye akajiunga na Real Madrid akaenda kulitwaa taji hilo mara tatu huku pia akiwa katika kikosi cha Ujerumani kilichobeba Kombe la Dunia mwaka 2014.

### #1. CRISTIANO RONALDO | MANCHESTER UNITED 2008, REAL MADRID 2014, 2016, 2017 & 2018

Katika zama za Ligi ya Mabingwa Ulaya, hakuna mchezaji yeyote alishinda taji hilo mara nyingi zaidi ya Cristiano Ronaldo. Raia huyu wa Ureno ameweka historia ya ufungaji mabao kwenye michuano hiyo, akiwa ametikisa nyavu mara 128, akianzia Manchester United, Real Madrid na Juventus.

Wakati Ronaldo akitengeneza jina lake na 'Mashetani Wekundu' na kushinda taji hilo chini ya Sir Alex Ferguson, Real Madrid ndiko alikopata mafanikio makubwa zaidi.

'Los Blancos' hao waliweka rekodi ya kumsajili Ronaldo mwaka 2009 na akawa mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani kutokea pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu ambako amelibeba taji hilo mara nne.


Kipindi cha majira ya joto mwaka 2018, Ronaldo alitangaza uamuzi wake wa kwenda kujiunga na Juventus.

## Nukuu

"Si mimi tu ninayesema hivyo. Messi [Lionel] anasema yeye mwenyewe, kwamba anataka kumaliza kipindi chake cha kucheza soka hapa Barcelona na ndio klabu pekee kwake, yupo wazi kabisa, amekuwa hapa tangu akiwa mtoto, anajua rangi yake na yeye ni sehemu ya historia ya klabu hii," **Rais wa Klabu ya Barcelona, Josep Maria Bartomeu.**



"Nafikiri...Jurgen Klopp (ndio kocha wangu bora) na baada ya hapo ni Pep Guardiola kwa asilimia 100. Klopp ana sura mbili. Unaweza kuona ni kama baba, lakini sehemu ya pili ni kama kocha. Anaweza kukuambia kila kitu – na sizungumzii kuhusu vitu vizuri  kuhusu vitu vibaya, pia kwa (wachezaji), ni mtu mwenye hamasa kubwa. Anafanya vizuri kwa sababu anajua wapi pakuwasukuma wachezaji na wapi pa kulegeza kidogo," **mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski**




"Kama ungeniuliza mimi swali hilo miaka miwili iliyopita, ningejibu (Ndio Madrid inaweza kupindua matokeo). Madrid wangekuwa na nafasi kubwa ya kushinda kama wengekuwa na Cristiano. Nyuma walikuwa na Cristiano, ambaye ni mashine ya kufunga mabao, anaweza kutengeneza tofauti dakika yoyote katika mchezo na ana uwezo kuipa timu mabao 50 kwa msimu mmoja," **mshambuliaji wa zamani wa Arsenal, Emmanuel Adebayor akiliambia AS kabla ya Real Madrid kutolewa na Manchester City Ligi Mabingwa Ulaya.**





# MABAO 756 LIGI KUU BARA YATIA FORA TUZO ZIKITOLEWA

Mgeni rasmi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo (kulia), akimkabidhi kiungo wa Simba, Clatous Chama tuzo ya Mchezaji Bora wa Ligi Kuu, Ijumaa iliyopita. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu msimu wa 2019/20, ikiwa imekamilika huku Jumamosi iliyopita kulikuwa na utoaji tuzo za wachezaji, makocha na waamuzi waliofanya vema msimu huu, kiungo wa Simba Clatous Chama akishinda tuzo mbili ya kiungo bora na mchezaji wa mwaka, jumla ya mabao 756 yamefungwa kwenye ligi msimu huu na kuweka rekodi ya kuwa na mabao mengi zaidi.

**Hata hivyo, kati ya mabao hayo 753 yameingia nyavuni, huku matatu yakiwa ya bure ambayo yalitokana na mechi kati ya Ruvu Shooting dhidi ya Prisons iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mabatini Februari 12, mwaka huu.**

Ni kwamba Prisons ilipata pointi tatu na mabao matatu kwa kanuni, kutokana na wenyeji Ruvu Shooting kushindwa kuleta gari la wagonjwa uwanjani. Msimu uliopita yalifungwa jumla ya mabao 738 kwenye Ligi Kuu, hivyo 18 yamezidi msimu huu.

Kwenye tuzo za Jumamosi, Chama wa Simba alishinda tuzo ya kiungo bora na mchezaji bora wa msimu, kipa wa Simba akishinda kipa bora wa msimu, huku Nicolaus Wadada wa Azam FC, akishinda tuzo ya beki bora wa mwaka.

Tuzo ya mchezaji bora chipukizi ilikwenda kwa mchezaji wa Biashara Novetus Dismas, Patson Shigala wa Mbeya City yeye akiwa ameshinda goli bora la msimu.

Ukiacha kwa wachezaji, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck alishinda tuzo ya kocha bora wa msimu uliomalizika, huku mwamuzi bora msimu huu ni Ramadhan Kayoko wa Dar es Salaam.

Wakati wachezaji, makocha na waamuzi wakipata tuzo zao, mwandishi wa makala haya anakuletea takwimu mbalimbali za Ligi Kuu iliyomalizika kwa mujibu wa rekodi zetu.

## MABAO 756 YATINGA

Kama ilivyotanguliwa hapo juu, Ligi Kuu msimu huu kumezaliwa jumla ya mabao 756 ambayo ni mengi zaidi tangu mfumo mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara uanzishwe msimu wa 2007/08. Hata hivyo, yanazidi 18 tu ya misimu miwili iliopita, 2018/19 yakifungwa 738, na msimu wa 2017/18 yakifungwa 600.

## WACHEZAJI 289 WALIVYOTUPIA NYAVUNI

Jumla ya wachezaji 289 ndiyo waliopachika idadi ya mabao 753 nyavuni, ambayo ukichanganya na matatu ya kupewa Prisons kama tulivyoeleza awali unapata idadi ya mabao 256. Idadi hii ya wachezaji pia ni kubwa kuliko ile ya msimu uliopita 2018/19 ambao ni wachezaji 243 ndiyo walifunga mabao 738. Hii inaonyesha kuwa msimu huu kuna ongezeko la wachezaji 46.

## PENALTI KIDUCHU MSIMU HUU

Ni msimu ambao penalti hazikuwa nyingi kama uliopita. Ni jumla ya penalti 38 tu. Msimu uliopita jumla ya penalti 52 zilipatikana. Ni pungufu ya penalti 14. Katika penalti 38 zilizopatikana msimu huu, 31 ziliwekwa kwenye kamba na saba ziliota mbawa.

Meddie Kagere ambaye ndiye mfungaji bora msimu huu kwa mabao 22, vile vile ndiye kinara wa kupachika mabao ya penalti, akiwa amefunga mabao sita, huku Peter Mapunda wa Mbeya City akifuatiwa akiwa amefunga mabao matano ya mikwaju ya penalti.

Wengine waliofunga penalti zaidi ya moja ni Awesu Awesu wa Kagera Sugar, Daruweshi Saliboko wa Lipuli na Wallace Kiango wa Mwadui, kila mmoja akifunga penalti mbili kati ya 31 zilizofungwa msimu huu.

Penalti saba zilizoota mbawa msimu huu zilikoswa na Said Hamisi na Waziri Junior wote wa Mbao FC, Sixtus Sabilo wa Polisi Tanzania, Benard Morrison wa Yanga, Kagere wa Simba, Issa Rashid wa Mtibwa Sugar na Paul Materazi wa Lipuli. Kati ya penalti 52 za msimu uliopita, 44 zilitinga kwenye kamba na nane zilikoswa.

## HAT-TRICK NANE ZAVUNJA REKODI

Kumekuwa na ongezeko la wachezaji kufunga mabao matatu kwenye mechi moja 'hat-trick' msimu huu. Jumla ya 'hat-trick' nane zimefungwa Ligi Kuu 2019/20, ikiwa ni ongezeko la 'hat-trick' mbili kwani, msimu uliopita 2018/19 zilikuwa sita.

Obrey Chirwa wa Azam FC, amepata 'hat-trick' mbili kwa msimu mmoja kama alivyofanya Emmanuel Okwi wa Simba msimu uliopita. Mbali na Chirwa kupata mbili, wengine waliofunga 'hat-trick' ni Ditram Nchimbi wakati huo akiwa Polisi Tanzania kabla ya kuhamia Yanga kipindi cha dirisha dogo, Saliboko wa Lipuli, Kelvin Sabato wa Kagera Sugar, David Richard wa Alliance, Kagere wa Simba, na Atupele Green wa Biashara.

Msimu uliopita, Okwi alifunga 'hat-trick' mbili, huku wengine wakiwa ni Alex Kitenge wa Stand United, Salum Aiyee wa Mwadui, Fully Maganga, na Kagere ambaye ameweka rekodi ya kufunga 'hat-trick' misimu miwili mfululizo, lakini akiwa mfungaji bora misimu miwili mfululizo pia.

## WACHEZAJI 18 WAJIFUNGA WENYEWE

Jumla ya wachezaji 18 wa Ligi Kuu Tanzania Bara, wameingia kwenye orodha ya wachezaji waliojifunga wenyewe kwa bahati mbaya, wakiwa kwenye harakati za kuokoa mipira langoni mwao, huku mchezaji David Nartey wa Singida United akiweka rekodi ya aina yake ya kujifunga mara mbili kwenye mechi mbili tofauti.

Alijifunga kwenye mechi dhidi ya Azam, timu yake ikibugizwa mabao 7-0, pia katika mechi dhidi ya Biashara, timu yake ikilala kwa mabao 2-0.

Wachezaji wengine waliojifunga ni Ibrahim Said wa Mbao FC, George Chota wa Mbeya City, Yassin Mustapha wa Polisi Tanzania, Dickson Daud wa Mtibwa Sugar, Mtenje Juma wa Coastal Union, Paul Bukaba wa Namungo, Geofrey Lucheke wa Alliance, Juma Nyosso wa Kagera Sugar, na Michael Ismail wa Prisons.

Wengine ni Ally Sonso na Lamine Moro wote wa Yanga, Augustino Samson wa Mwadui, Issai Kauju wa Lipuli, Henry Joseph wa Mtibwa Sugar, Idd Mobby wa Polisi na Jumanne El Fadhili wa Prisons.

**JE, WAJUA?**



CLARENCE Seedorf ni mchezaji pekee kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kushinda taji hilo akiwa na timu tatu tofauti. Hadi anastaafu kucheza soka, Mholanzi huyo amebeba taji hilo mara nne, alilibeba akiwa na Ajax mwaka 1995, Real Madrid 1998, AC Milan 2003 na 2007.



# Waziri ataka vyakula vya madini ya folic acid kwa wasichana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ametaka fedha zinazotumika kununua vidonge vya asidi ya foliki (Folic acid) kwa wanafunzi na wasichana balehe kuanzisha bustani shuleni ili kuzalisha vyakula vinavyotoa madini hayo.

Waziri Ummy akizindua Siku ya Lishe na Maadhimisho ya Lishe Kitaifa jijini hapa, mwishoni mwa wiki, alishauri vidonge hivyo viendelee kutolewa kwa wajawazito na wanawake walio katika umri wa kuzaa. "Fedha ambazo zinatolewa na wadau wa maendeleo kwa ajili ya kununua vidonge vya folic acid zitumike kuanzisha bustani shuleni kwa ajili ya kuzalisha maboga na matunda mengine ambayo yanazalisha asidi hiyo badala ya kutoa vidonge," alisema.

"Kuanzisha bustani vijana watapata ajira na wataongeza kipato ya vijana, lakini pia watakuwa wamezalisha vyakula vyenye asidi ya foliki ili kusaidia wanafunzi badala ya vidonge," alisema.

Akizungumzia kuhusu unywaji wa maziwa shuleni, Waziri Ummy alisema atamwandikia barua Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ya kutoa pendekezo kuanzia Septemba mosi mwaka huu kila shule iwe na kibanda cha maziwa.

Alisema hajapiga marufuku uuzaji wa vyakula vingine shuleni, lakini ataomba katika kila shule hasa za bweni lazima ziwe na kibanda kimoja cha maziwa na kutumia fedha wanazopewa na wazazi kununua maziwa shuleni na kupata lishe bora. Ummy alisema, kuanzisha vibanda vya maziwa shuleni hasa shule za kutwa, kutasaidia wanafunzi kuboresha afya yao, lakini kwa tasnia na maziwa kutasaidia kupanua soko la bidhaa yao na kuongeza kipato.

Alisema utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unaonyesha kwamba kila mtu anatakiwa kunywa nusu lita ya maziwa sawa na lita 180 kwa mwaka, lakini kwa sasa kila mtu anakunywa lita 40 kwa mwaka sawa na vijiko 10 vya chai kwa siku.

Aliitaka Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) kuharakisha mwongozo sahihi wa uandaaji vyakula vya nyongeza kwa watoto vyenye virutubisho, ambao unaandaliwa na taasisi hiyo kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kupitia ufadhili wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

Kuhusu udumavu wa watoto wa chini ya miaka mitano, waziri huyo alisema umepungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2014 hadi asilimia 31.8 mwaka juzi, lakini kasi bado haitoshi inatakiwa kufanyika zaidi.

Aidha, aliomba kuongeza kasi ya kupunguza tatizo la wanawake kuongezeka uzito na viribatumbo kwa walio katika umri wa kuanza kuzaa, ambapo takwimu zinaonyesha kwa mwaka 2014 kulikuwa na asilimia 29.7 ya wanawake hao na imeongezeka na kufikia asilimia 31.7 mwaka 2018.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Dorothy Gwajima, alisema kwa mwaka 2017/18 serikali ilianza kutenga fedha kwa ajili ya lishe. Alisema kwa mwaka huo zilipatikana Sh. bilioni tisa na zikatumika asilimia 30 tu, 2018/19 zilitengwa Sh. bilioni 15 zikatumika asilimia 45.

"Bajeti ya 2019/20 zilitengwa Sh. bilioni 16.7 na zikatumika asilimia 70, kitendo kinachoonyesha utekelezaji wa afua za lishe ulizidi kuongezeka, lakini 2020/21 fedha zilizotengwa zimepungua hadi Sh. bilioni 12, hata hivyo uwekezaji wa ndani kuhusu lishe umeongezeka kutoka Sh. bilioni 9 hadi 11," alisema.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene (kulia mwenye suti nyeusi), akimsikiliza Meneja wa Kampuni ya Premium Active Tanzania (LTD) inayotengeneza nishati mbadala ya mkaa mweupe kwa kutumia bidhaa ya nyasi, Aristotle Nikitas, alipotembelea banda lao katika maonyesho ya Nanenane viwanja vya Nzuguni, Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# NEC yashauriwa kusimamia sheria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetakiwa kuhakikisha inasimamia sheria kwenye mchakato wa uchaguzi unaoendelea nchini na kuwachukulia hatua wanaokiuka taratibu zilizowekwa.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, alisema hayo jana alipotembelea banda la Tume hiyo kwenye maonyesho ya wakulima yanayofanyika katika viwanja vya Nane nane Nzuguni jijini hapa.

Alisema kuna baadhi ya wagombea wamekuwa wakikiuka taratibu zilizowekwa.

"Kazi kubwa inafanyika lakini kazi iliyo mbele ni ngumu kwani kuna watu wanagombea kwa kufuata taratibu, lakini wengine sivyo, kuna maneno ya ovyo ovyo, kuchafuana hata kabla ya kuchukua fomu za uteuzi mambo mengi yanaonekana, mkiona faulo za wazi wazi mchukue hatua hata vyombo vya sheria vichukue hatua ili uchaguzi uwe wa haki," alisema.

Kadhalika, alisema kuna haja ya kuhakikisha elimu wanazotoa zinawafikia wananchi waliopo vijijini na makundi mbalimbali ikiwamo wajasiriamali na watu wenye ulemavu.

Alisema Taifa linakwenda kufanya maamuzi magumu kwa kuchagua kiongozi anayefaa kuliongoza taifa.

"Taifa linakwenda kufanya maamuzi magumu ya nchi yetu sio maamuzi ya mtu ni maamuzi ya hatima ya taifa, tukachague kiongozi mwenye mapenzi mema na nchi yetu atakayelifanya taifa lizidi kusonga mbele," alisema.

Alisema kila mmoja anatakiwa kuzingatia kanuni na taratibu na wananchi wasikubali kutumika na kikundi chochote kwa kufanya mambo yanayohatarisha amani.

Alivitaka vyama vya siasa kuheshimu sheria za nchi ili uchaguzi ufanyike kwa haki na amani.

Kwa upande wake, Ofisa Elimu Idara ya Habari na Elimu kwa Mpigakura, Johari Mutani, alisema Tume imejipanga katika maandalizi ya uchaguzi mkuu mwaka huu.

"Tulifanya uboreshaji wa daftari awamu ya kwanza, kisha awamu ya pili, uchakataji wa taarifa za daftari ukawa unaendelea sasa tume itaanza kutoa fomu kwa wagombea wa ubunge na udiwani Agosti 12, mwaka huu," alisema.

Alisema wanaendelea kuwafikia wananchi kutoa elimu kwa njia mbalimbali, ikiwamo matangazo, vipindi vya redio na kukutana moja kwa moja na wapigakura.

Kwa Mujibu wa Ratiba iliyotolewa na NEC, uchaguzi wa Rais wabunge na madiwani utafanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Fomu za uteuzi kwa wagombea wa kiti ya Rais na Makamu wa Rais zimeanza kutolewa na mwisho ni Agosti, 25 mwaka huu, huku za wagombea ubunge, uwakilishi na udiwani zitaanza kutolewa Agosti 12 hadi Agosti 25 mwaka huu katika ofisi za halmashauri husika na ofisi za kata.

Kampeni za uchaguzi zitaanza Agosti 26 na hadi Oktoba 27, mwaka huu.

# Wauzaji wa bidhaa wasiosajili majengo watangaziwa kiama

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), Kanda ya Kati limesema halitasita kuwachukulia hatua za kisheria wauzaji wote wa bidhaa kwenye maduka mbalimbali ambao hawajasajili majengo yao.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kaimu Mkuu wa Kanda ya Kati Dodoma wa Shirika hilo, Salome Emanuel, katika maonyesho ya Nanenane katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Alibainisha kuwa shirika hilo lina jukumu kusajili majengo hayo na bidhaa zinazotoka nje ya nchini, ambalo limekasimiwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Namba 8 ya Mwaka 2019.

"Shirika linafanya ukaguzi na usajili wa majengo hayo kupitia mifumo rahisi, ambapo mwombaji anatakiwa kufanya maombi ya kupata usajili huo kupitia mifumo yetu na anapatiwa namba kwa ajili ya kufanya malipo na baadaye tathmini inafanyika na jengo linasajiliwa," alisema.

Alisema ni muhimu wafanyabiashara hao wakasajili majengo yao kwa kuwa kinyume na hapo sheria zitachukuliwa.

"Pia wanaoingiza bidhaa tunawashauri wafanye usajili wa bidhaa zao ili kuepuka kukutana na faini mbalimbali kwa kutokufuata na kuzingatia sheria," alisema.

Alifafanua kuwa shirika hilo limepewa majukumu yake kwa mujibu wa sheria namba 2 ya viwango ya mwaka 2019 na linafanya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ikiwamo utengenezaji wa viwango.

"Pia utekelezaji katika mifumo mbalimbali ambayo imewekwa scheme ya uthibiti ubora pamoja na uthibitishaji wa ubora wa bidhaa, pia inafanya utekelezaji wa upimaji wa sampuli mbalimbali na uhakiki wa ubora wa vipimo vinavyotumika," alisema.





## Serikali yaahidi amani uchaguzi mkuu Oktoba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakuu wa Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameahidi kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu unafanyika kwa amani na utulivu na kwamba yeyote atakayefanya vurugu atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Walitoa ahadi hiyo walipokuwa wanatoa salamu za mikoa yao kwenye kilele cha Manoyesho ya Wakulima (Nanenane) ambayo kikanda yalifanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya na kufungwa na Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa. Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Mstaafu Nocodemas Mwangela, alisema atahakikisha uchaguzi huo unafanyika bila vurugu za aina yoyote, huku akisisitiza kuwa uchaguzi huo utakuwa tofauti na uliofanyika mwaka 2015. Aliwataka wanasiasa kujiandaa kufanya siasa za kistaarabu ambazo zitajikita katika sera badala ya kuvuruga amani akisisitiza kuwa yeyote atakayefanya tofauti na matakwa ya sheria atashughulikiwa.

"Tunataka uchaguzi ambao utakuwa wa haki na amani ili washindi wa nafasi zote wapatikane kwa haki, hatutataka mwanasiasa yeyote kufanya siasa za matusi na lugha chafu dhidi ya wengine na atakayejaribu tutamfundisha," alisema Brig. Mwangela. Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alisema amejipanga na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika bila kuwapo kwa fujo za aina yoyote.

Alisema katika mkoa wake atahakikisha watu wote wanaoshiriki kwenye siasa anashiriki kwa uhuru bila kuzuiliwa na mtu mwingine na kwamba atakayezuiliwa ni yule atakayefanya mambo yasiyokidhi matakwa ya kisheria.

# Wakuu wa mikoa kutafiti udumavu Nyanda za Juu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKUU wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameagizwa kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha kuwa na kiwango kikubwa cha udumavu wa watoto licha ya mikoa hiyo kuongoza nchini kwenye uzalishaji wa chakula.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitoa agizo hilo juzi kupitia hotuba yake ambayo ilisomwa kwa niaba yake na Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, wakati wa kilele cha Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) ambayo kwa mikoa ya ukanda huo yalifanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Akisoma hotuba hiyo, Dk. Tulia alisema kiwango cha udumavu wa watoto kwenye mikoa hiyo ni asilimia 42.9 wakati kiwango cha kitaifa ni asilimia 31.8, na kwamba sababu za kiwango hicho kuwa kikubwa hazieleweki mpaka sasa.

Alisema kiwango cha uzalishaji wa mazao mbalimbali katika mikoa hiyo kwa msimu wa kilimo uliopita kilikuwa tani milioni 11.4 na ziada ya chakula mpaka sasa ni asilimia 201 na hivyo akadai kuwa hakuna sababu ya watoto kukabiliwa na udumavu. "Sasa nawaagiza wakuu wa mikoa yote ya ukanda huu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, muanze mikakati ya kukabiliana na tatizo hili kwa kufanya utafiti wa kina na mkijua chanzo itakuwa rahisi kukabiliana nalo na haraka hatua zichukuliwe maana hii ni aibu," alisema Dk. Tulia. Alisema wakati alipokuwa anakagua mabanda ya maonyesho alibaini kuwa mikoa hiyo inazalisha mazao ya aina mbalimbali yakiwamo yenye virutubisho ambavyo vinasaidia kukabiliana na udumavu kwa watoto.

Aliwataka viongozi wote kuhakikisha teknolojia za kilimo, ufugaji na uvuvi zilizokuwa zinaonyeshwa kwenye maonyesho hayo kusambaa kwa wananchi ili waongeze uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa ajili ya chakula na malighafi kwa ajili ya viwanda.

Katika hatua nyingine, Dk. Tulia alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege na miundombinu ya usafiri wa majini ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya wakulima na bidhaa zitokanazo na mazao hayo kwenda sokoni.

"Lakini serikali inaendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao mbalimbali, pia kwa mikoa hii tutajenga vyumba vya baridi kwa ajili ya kuhifadhi matunda na mboga kabla ya kusafirisha nje ya nchi kwenda kuuzwa," alisema Dk. Tulia. Vilevile, alisema serikali inaendelea kuweka mkazo kwenye uboreshaji wa mazao ya kimkakati ikiwamo chai, kahawa, pamba, korosho, maparachichi na mazao mengine ili kuhakikisha wakulima wanazalisha kwa tija zaidi.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa mikoa saba ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema watahakikisha wanatekeleza maelekezo yote ya serikali ili kufikia malengo yaliyowekwa. Alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwamo Sh. bilioni 18 kwa ajili ya uwekaji wa taa na miundombinu mingine katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inaongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini, hali ambayo iliifanya ibatizwe jina la Ghala la Taifa la Chakula, lakini bado mikoa hiyo inakabiliwa na tatizo la udumavu wa watoto.



Mmoja wa askari polisi wa Mkoa wa Mbeya Kitengo cha Usalama Barabarani (kushoto), akitoa elimu ya usalama barabarani kwa wananchi wakati wa maonyesho ya Nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kijana anayedaiwa kuuawa na askari TANAPA azikwa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MFUGAJI Ulandi Dotto (28), mkazi wa Kijiji cha Mwanavala wilayani Mbarali, anayedaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi na askari wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) wakati akipitisha mifugo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, amezikwa, huku wafugaji wakishauriwa kutolipa kisasi.

Aidha, wafugaji hao wameaswa kutoichukia TANAPA kwa maelezo kuwa askari waliofanya mauaji hao ni wahalifu kama wahalifu wengine, hivyo wafugaji wanatakiwa wawe watulivu wakati vyombo vya dola vikishughulikia jambo hilo.

Akizungumza wakati wa mazishi ya kijana huyo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki kijijini kwao Mwanavala katika Kata ya Imalilo-Songwe wilayani Mbarali, Mwenyekiti wa Chama cha wafugaji Taifa, John Wambura, alisema chama hicho kitahakikisha haki inatendeka.

Alisema yeye kama kiongozi mkuu wa chama hicho hatakuwa tayari kushuhudia wafugaji wakilipa kisasi dhidi ya maaskari waliotekeleza tukio hilo la mauaji na badala yake kila mmoja atatakiwa kuzingatia sheria.

"Mmesema hapa kwamba tukio hili ni la tano kutokea katika wilaya hii, tunajua hakuna fidia ya uhai wa mwanadamu lakini angalau serikali itowe kifuta machozi, niwahakikishie kwamba hawa maaskari lazima mtawaona mahakamani," alisema Wambura.

Alisema viongozi wa juu wa chama cha wafugaji nchini watahakikisha wanashirikiana na familia ya marehemu ili kuhakikisha haki inatendeka na familia hiyo inapata haki yake.

Baba mzazi wa kijana huyo, Mzee Dotto Shigela, aliwaomba wadau kumsaidia ili familia yake ipate haki kwa maelezo kuwa marehemu ameacha mke na watoto wawili, ambao watahitaji kupata malezi bora.

Alisema marehemu ndiye alikuwa mtoto wake wa kwanza na alikuwa msaada mkubwa kwenye familia, hivyo akadai kuwa maisha ya wanafamilia hao watayumba kutokana na kutokuwapo kwa kijana huyo. "Nililalamika kwa RPC maana walianza kupindisha wakati tunaandikisha, walianza kudai kuwa risasi iliingilia kifuani wakati ukweli ni kwamba risasi iliingilia mgongoni na ikatokea kifuani, hivyo naomba sana haki itendeke kwenye tukio hili," alisema Shigela.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambaye ni ofisa mifugo wa wilaya hiyo, Augustino Lawi, alisema serikali inawathamini na inahitaji sekta ya mifugo iendelee kustawi kutokana na kuwa miongoni mwa sekta zinazoingizia mapato mengi.

Lawi alisema sekta ya mifugo ni ya pili kwa kuiingizia mapato halmashauri hiyo baada ya sekta ya kilimo ambayo ndiyo inayoongoza kwa kuingiza mapato.

"Tatizo ni kwamba ufugaji wetu utategemea sana malisho ya asili kama wanyama wengine hali ambayo imekuwa ikisababisha migogoro, sasa hivi tuna dhamira ya kubadili ufugaji kwa kuanza kuzalisha malisho ili tuondoe huu uhaba wa malisho," alisema Lawi.

Mwanasheria wa Chama cha wafugaji nchini, Glorious Luoga, aliwataka wafugaji kuhakikisha kuwa wakati wanadai haki pia wazingatie sheria za nchi ili kuepuka migogoro isiyokuwa na ulazima.

Alisema moja kati ya taratibu wanazostahili kuzingatia ni kuepuka kuingiza mifugo kwenye hifadhi na kwamba ni wajibu wa wafugaji kuzingatia utaratibu huo na kwamba hakuna haki bila wajibu.





Khatib Suleiman akiangalia bidhaa za wajasiriamali katika maonyesho ya Nanenane yaliyofanyika Dole Wilaya ya Magharibi A Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Shein aitaka wizara kuandaa mwelekeo wa kituo umeme jua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto ina jukumu la kukaa pamoja na uongozi wa kituo cha wanawake kinachotengeneza vifaa vya umeme wa jua (Barefoot College), ili kuandaa mwelekeo wa kituo hicho baada ya kukamilika kipindi cha miaka mitano tangu kifunguliwe.

Dk. Shein alisema hayo jana Kinyasini, Mkoa wa Kaskazini Unguja katika sherehe za kutimiza miaka mitano tangu kuanzishwa kwa kituo hicho pamoja na ufunguzi wa jengo jipya la dakhalia kwa ajili ya wanafunzi.

Alisema kwa kuzingatia sera na maelekezo ya serikali, wizara hiyo inapaswa kukaa pamoja na uongozi wa kituo hicho na kuanza kufikiria mahitaji ya baadaye ya kituo, ikiwamo eneo la ardhi litakalotumika kwa ajili kuongeza majengo na baadhi ya nyenzo muhimu zitakazohitajika.

Alisema kuwapo kwa changamoto mbalimbali, ikiwamo uhaba wa madarasa na maabara ya kufundishia, kwa ajili ya washiriki wengi wa mafunzo pamoja na ukosefu wa lami katika eneo dogo la barabara inayoingia kituoni hapo ni mambo yanayohitaji kutafutiwa ufumbuzi na wizara hiyo.

"Nauagiza uongozi wa wizara uchukue hatua ya kuzitatua changamoto hizo, zile zilizomo ndani ya uwezo wao moja kwa moja na zile zinazohitaji ushirikiano na taasisi nyingine wazishughulikie," alisema. Alisema kuna umuhimu wa kukiendeleza kituo hicho kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira ya Zanzibar na mabadiliko ya dunia.

Dk. Shein aliuagiza uongozi wa kituo hicho kuunda jumuiya ya wanafunzi wanaomaliza mafunzo kituoni hapo na kutoa mialiko ya kufika kituoni ili kueleza walivyofaidika na mafunzo, jinsi wanavyoitumia taaluma waliyoipata na mafanikio yao.

Alisema kuwa kuna mafanikio makubwa yaliyopatikana na kituo hicho ndani ya kipindi cha miaka mitano na kuwashukuru wote waliochangia kufanikisha uendeshaji mzuri wa kituo hicho.

Alisisitiza umuhimu wa viongozi wa kituo hicho kuwa na utaratibu mzuri wa kutunza na kuweka kumbukumbu za historia ya kituo hicho. Alisema ni jambo la kujivunia kuona kituo hicho kinapokea wanafunzi kutoka Tanzania Bara na nchi za jirani, na kubainisha kuwa hilo ndio lengo la serikali tangu kituo hicho kilipoanzishwa.

Naye Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, alisema wizara hiyo itaendelea na juhudi za kukiendeleza kituo hicho ili kufanikisha dhamira ya kuanzishwa kwake.

Naye, Balozi mdogo wa India nchini, Bhagwant Singh, alisema Serikali ya India itaendelea kuunga mkono juhudi za kukiimarisha kituo hicho ili kupata mafanikio makubwa.

Alisema ana matumaini makubwa kuwa ushirikiano uliopo kati ya India na Tanzania kwa ujumla utaendelea kuimarika kwa maslahi ya watu wa nchi mbili hizo.

Katibu Mkuu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Fatma Gharib Bilali, alisema jumla ya kinamama 45 wamenufaika kutokana na mafunzo ya utengenezaji wa vifaa vya umeme wa jua, ikiwamo 13 waliopata mafunzo hayo nchini India na sasa ni wakufunzi wa kituo hicho.

Mkuu wa kituo cha Barefoot College, Pendo alisema pamoja na mafanikio makubwa yaliopatikana katika uendeshaji wa kituo hicho, kuchelewa kupatikana vifaa vya umeme wa jua ni miongoni mwa changamoto zinazokikabili kituo hicho.

# Makatibu Tawala watakiwa kusimamia ugatuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKATIBU Tawala wasaidizi wametakiwa kusimamia vyema dhana ya ugatuzi na mfumo wa serikali za mitaaa kwa kuondoa matatizo yanayowakabili wananchi katika maeneo yao na kusimamia maendeleo ya mikoa.

Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema hayo wakati akifungua mkutano wa makatibu tawala wasaidizi wa mikoa mitatu ya Unguja uliofanyika katika ofisi yake Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja

Alisema kuwa Serikali Kuu imeanzisha ugatuzi na kushusha madaraka katika serikali za mitaa kwa lengo la kuandaa na kupanga miradi ya maendeleo na kupunguza changamoto zinazowakabili kwa wepesi zaidi.

Kadhalika, alisema endapo watafuta mifumo iliyowekwa na Serikali Kuu kuhusu azma ya kuanzishwa mfumo wa ugatuzi katika mikoa na kuwashauri viongozi serikali za mitaa na mkoa changamoto zinazo wakabili wananchi.

Mkuu wa mkoa aliwataka makatibu tawala wasaidizi kujua wajibu wao na kutimiza majukumu yao ya kazi bila kuvunja sheria na utaratibu za utendaji na kubuni mipango ya kuletea maendeleo ya mkoa.

"Lazima mfanye kazi kwa vitendo kwa maslahi ya taifa ili nchi iweze kupata maendeleo," alisema. Mwenyekiti wa kikao hicho, Fakih Kombo Fakih, alisema mpango huo wa pamoja wa kushirikisha makatibu tawala wasaidizi wote wa Unguja unalengo la kubadilishana uzoefu mbinu na kuibua mikakati bora ya utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Makatibu Tawala Wasaidizi walisema hatua hiyo waliyoianzisha ya kukutana kila baada ya miezi mitatu itasaidia kwa kiasi kikubwa kutaleta mabadiliko katika utendaji wa kazi zao licha ya kukumbwa na uhaba wa vitendea kazi ikiwamo usafiri wa uhakika.

Waliishauri serikali kuona umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa masheha kuanzishwa kwa mfumo huo, ambao kwa sasa inaonekana hakuna uelewa wa kutosha kwa jamii ili waweze kutoa ushirikiano katika masuala mbalimbali ikiwamo ya vitendo vya udhalilishaji.

# Wajasiriamali waomba kuongezwa maonyesho zaidi ya bidhaa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJASIRIAMALI mbalimbali wanaoshiriki maonyesho ya Siku ya Wakulima Nanenane huko Kizimbani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, wameiomba serikali kuongeza maonyesho mengine zaidi ili kutoa nafasi ya kuonyesha bidhaa wanazozalisha na kupata soko kwa ajili ya kuongeza kipato.

Akizungumza na Nipashe, mjasiriamali Wache Makame Simai wa kijiji cha Banda maji, Chaani Mkoa wa Kaskazini Unguja, anayetengeneza sabuni kwa kutumia malighafi asilia, alisema wamefurahishwa kuwapo kwa maonyesho hayo ambayo yametoa fursa kwa wajasiriamali kuonyesha bidhaa mbalimbali wanazozizalisha.

Alisema anatengeneza sabuni zinazotokana na malighafi ya mti wa mkaratusi na karafuu ambayo hutoa tiba ya magonjwa ya ngozi.

Alisema ni mara yake ya kwanza kushiriki maonyesho hayo ambayo yamempa fursa kubwa ya kuonyesha bidhaa zake na kuzitangaza katika soko.

"Hii ni mara yangu ya kwanza kuhudhuria maonyesho kama haya, nimetengeneza bidhaa mbalimbali ikiwamo sabuni zinazotokana na malighafi ya karafuu pamoja na makonyo ambayo ni sehemu ya tiba kwa binadamu," alisema.

Naye mjasiriamali Time Kombo, alisema ameanza kutengeneza unga wa mronge kwa matumizi ya chakula ukiwa ni lishe nzuri pamoja na tiba kwa maradhi mbalimbali na husaidia kuondoa gesi mwilini na usafishaji wa figo.

"Nimeanza kutengeneza unga wa mronge ambao unatokana na majani hii ni mjarabu kwa kutibu maradhi mbalimbali ikiwamo kuondoa gesi na kusafisha figo na kushusha sukari mwilini," alisema.

Ofisa Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), Nairat Abdalla Ali, alisema wajasiriamali 1,609 wamewezeshwa kiuchumi kupitia mradi wa WEZA namba tatu ambao lengo lake kubwa ni kuwapatia mafunzo wajasiriamali kufikia malengo ya kujitegemea.

Alisema mradi huo ambao unafadhiliwa na Milele Foundation, umepata mafanikio makubwa kwa wajasiriamali kutengeneza na kuzalisha bidhaa za mikono ikiwamo kusuka mikoba ya ukili, pamoja na kutengeneza sabuni za maji na kuingia katika soko kwa mafanikio makubwa.

Mratibu wa Milele Foundation, Alice Mushi, alisema wataendelea na mikakati yao ya kuwaunga mkono wajasiriamali kuzalisha bidhaa na kuingiza kipato.

Maonyesho hayo yameshirikisha taasisi 120 ikiwamo wajasiriamali kutoka Unguja na Pemba.

# NMB yatakiwa kuwekeza kwenye elimu kuleta tija sekta ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka Benki ya NMB kuendelea kuongeza nguvu zaidi kwa wafugaji, wakulima, wavuvi kuwapa elimu ya jinsi gani wanaweza kupata tija kwenye shughuli zao.

Majaliwa ameipongeza benki hiyo kwa kuendelea kutoa elimu ya kifedha kwa wananchi walioko kwenye sekta ya kilimo, ambapo ameishauri kutoa elimu ya jinsi gani wanaweza kuongeza tija.

Alitoa wito huo baada ya kutembelea banda la benki hiyo, wakati wa kilele cha maonyesho ya Nanenane kwenye viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu.

Alisema mkulima afundishwe jinsi gani anaweza kuzalisha kwa tija kulingana na eneo alilonalo kama ni mkulima, lakini kama ni mfugaji naye afundishwe kulingana na mifugo aliyonayo.

“Kama ni mfugaji mpigieni mahesabu kulingana na mifugo yake na kama ni mkulima hata akiwa na hekari moja mpigieni mahesabu yote tangu analima, parizi, dawa, mbegu,” alisema Majaliwa.

“Akipigiwa hizo hesabu zote ambazo ataweza kuzitumia kwenye shughuli zake, yeye ataona faida atapata kiasi gani na anaweza kukopa kiasi gani kwenye benki, mkifanya hivyo mtawavutia wengi zaidi na wataona kumbe inawezekana,” aliongeza Majaliwa.

Alisema kuwa elimu hiyo itolewe kulingana na mhusika anavyotaka kulingana na raslimali alizonazo na anaweza kuzitumia vipi kupata faida ikiwa ataamua kuzalisha kwa tija.

“Kadri mfugaji wa ng'ombe alionao kama ni watano, mpigieni hesabu ili aweze kufuga kwa tija na akikopa anaweza kupata faida na kulipa huo mkono, anzieni mahesabu ya chini, msiwapeleke kwenye hesabu kubwa,” alisema Majaliwa.

Akitoa maelezo kwa kiongozi huyo Ofisa Mkuu wateja binafsi na biashara, Filbert Mponzi, alimshukuru Waziri Mkuu kwa ushauri huo, ambapo alisema benki ya NMB imeupokea na itatekeleza.

Alisema kuwa benki hiyo imetumia maonyesho ya Nanenane yanayoendelea kwenda kanda mbalimbali nchi nzima kutoa elimu juu ya masuala ya kifedha kwa wakulima mbalimbali. Alisema lengo la elimu hiyo ni kuhakikisha wanapata mafunzo yatakayowawezesha kutunza fedha zao vizuri, kukuza mitaji ya kilimo, kulinda mazao yao kupitia bima zinazopatikana kwenye benki hiyo pamoja na fursa za mikopo ya kilimo.

“NMB inatambua kwamba ili mtu aweze kuimarika kifedha ni lazima ajenge mtazamo unaofaa kuhusu matumizi ya fedha, katika maonyesho haya tumeweza kutoa mafunzo kwa viongozi wa AMCOS 52,700 ambao nao wamewafikia wakulima 141,060,” alisema Mponzi.



Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Briedia Jenerali Wilbert Ibuge, akizungumza na waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam, kuhusu Mkutano wa 40 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), unaotarajiwa kufanyika Agosti 17, mwaka huu kwa njia ya mtandao Ikulu Chamwino jijini Dodoma. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Wanawake wafanikisha tohara 700, wafichua waume zao

**Na Thobias Mwanakatwe**

WILAYA ya Songwe imepata mafanikio makubwa ya kuwafanyia tohara wanaume zaidi ya 700 kwa kipindi kifupi kutokana na wanawake wilayani humo kuwafichua wenza wao ambao hawajatahiriwa.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Eggyfed Mwingiliela, akizungumza na gazeti hili juzi, alisema zoezi hilo ambalo linaendeshwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, limeonyesha mafanikio makubwa kutokana na ushirikiano mkubwa unaotolewa na wanawake kwa kuwafichua wenza wao.

Alisema katika kipindi cha wiki mbili tangu zoezi hilo limeanza zaidi ya wanaume 700 wamejitokeza na kufanyiwa tohara katika wilaya hiyo ambayo sehemu kubwa ya wakazi wake ni watu wanaojishughulisha na kazi za ufugaji, uchimbaji madini na uvuvi.

Mwingiliela alisema wizara iliamua kuendesha operesheni maalum katika wilaya hiyo kuwafanyia tohara wanaume kwa lengo la kupambana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi na saratani ya shingo ya kizazi.

“Wanawake wana uelewa mkubwa juu ya madhara yanayoweza kujitokeza endapo waume au wenza wao wasipofanyiwa tohara, hivyo wamekuwa mstari wa mbele kutoa taarifa za siri za wenza wao,” alisema.

Alisema mila na desturi za wakazi wa Wilaya ya Songwe umechangia kwa kiasi kikubwa wanaume wengi kuchelewa kufanyiwa tohara jambo ambalo limechangia ongezeko la maambukizi ya Ukimwi.

Alisema zoezi hilo linaendeshwa katika vituo vya afya vitatu vya Mbala, Saza na Hospitali ya Mwambani, iliyopo mjini Mkwajuni.

Tohara ni njia ya kitaalamu ya kuondoa ngozi ya juu ya uume ambayo mwanaume huzaliwa nayo na madhara ambayo mtu hajatahiriwa huyapata ni pamoja na kupata magonjwa ya zinaa na Ukimwi.

Utafiti uliofanywa na wataalamu unaonyesha kuwa kutahiriwa kunazuia kupata Ukimwi kwa zaidi ya asilimia 80.

Madhara mengine ni kupata kansa ya kizazi, mwanaume ambaye analala na mwanamke ambaye hajatahiriwa anakua kwenye hatari kubwa ya kumsababishia kansa ya mlango wa uzazi mwanamke husika.

Pia husababisha magonjwa ya njia ya mkojo; magonjwa ya njia ya mkojo (UTI) husababishwa na uchafua ambao hujificha ndani ya uume na kupita katikati ya tundu la uume hadi kwenye kibofu cha mkojo na kusababisha madhara makubwa.

# Wadau wataka kamati mitaani kuzuia ukatili

**Na Elizabeth Zaya**

WANAWAKE na wadau wanaoshughulikia masuala ya watoto, wameomba kuundwa kwa kamati za kuzuia ukatili katika mitaa na vijiji ili kuimarisha juhudi za kupambana na vitendo hivyo nchini.

Wakizungumza wakati wa mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, wadau hao pia walisisitiza umuhimu wa kuongeza ushiriki wa wanaume katika mapambano dhidi ya vitendo hivyo katika jamii.

“Ni wakati mwafaka wa kuunda kamati za kupambana na vitendo vya ukatili ambavyo vinaripotiwa kukithiri kila siku katika jamii, vijiji na mitaa, na kuna umuhimu wa kuwashirikisha viongozi wa mitaa kusukuma mbele juhudi za kupambana na vitendo hivi,” alisema Malcela Lungu, Mkurugenzi wa Shirika la Mabadiliko na Kujenga Ushirikiano kwa Wote (TIBA).

Alisema ushiriki wa wanaume katika mapambano dhidi ya vitendo hivyo haujaonekana, na kwamba kuanzishwa kwa kamati hizo kutasaidia kuongeza zaidi elimu ya ufahamu juu ya vitendo hivyo vya ukatili.

“Kama wadau, tunalazimika kukaa chini na kujiuliza ni jinsi gani tutafanya kazi kwa pamoja, tuimarishe juhudi za kuhakikisha kuwa tunapambana na vitendo hivi kwa nguvu zote vinavyoendelea kufanyika katika jamii.

Lungu alisema kuwa hadi sasa TIBA imefanya mipango ya uhamasishaji katika kata na mitaa mbalimbali ya Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam na kwamba wamepanga kuendelea kutoa elimu katika maeneo mengine ikiwamo katika vikundi mbalimbali na katika makundi ya watu wanaojikusanya kwenye vibanda vya kahawa.

Michael Sungusia, mtaalamu wa mambo ya jinsia, alisema kunahitajika mipango madhubuti zaidi ya uhamasishaji katika kushughulikia suala hilo.

“Tunapaswa kufanya kazi kwa pamoja mpaka ifike wakati tuone juhudi na matokeo mazuri kwa jamii yetu tunayoihudumia na tunaokoa maisha ya wanawake, watoto na wasichana ambao ndio waathirika wakubwa,” alisema Sungusia.

## HABARI KIMATAIFA

# Walioambukizwa corona Afrika wafikia milioni moja

**AFRIKA**

TAKWIMU zilizotolewa na Shirika la Habari la Reuters zimeonyesha kuwa bara la Afrika limerekodi visa milioni moja vya maambukizi ya virusi vya corona.

Pia imeonyesha idadi ya watu waliofariki kutokana na ugonjwa huo ni 21,983, waliopona wakifikia 676,395.

Vilevile, imeonyesha kuwa mfumo wa afya wa Afrika Kusini unaelekea kuzidiwa kutokana na idadi kubwa ya visa vya ugonjwa wa corona, uhaba wa vitanda vya wagonjwa pamoja na wahudumu wa afya.

Afrika Kusini ambayo ni nchi ya tano katika mataifa yalioathirika zaidi na virusi vya corona kote duniani, imerekodi zaidi ya nusu ya maambukizi yote barani Afrika.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Afrika Kusini, tangu kuripoti kisa chake cha kwanza Machi 5, mwaka huu nchi hiyo imerekodi visa 538,184 vya ugonjwa wa corona hadi kufikia juzi.

Hata hivyo, wataalamu wanasema huenda idadi ya maambukizi barani humo ni kubwa zaidi ikilinganisha na idadi inayoripotiwa.

Wanasema hii ni kutokana na mataifa mengi barani Afrika isipokuwa Afrika Kusini kukosa vifaa vya kutosha kufanya vipimo vya virusi vya corona na kueleza kuwa huenda bado kuna visa vingi ambavyo havijagunduliwa barani humo.

**Afrika Kusini ambayo ni nchi ya tano katika mataifa yalioathirika zaidi na virusi vya corona kote duniani, imerekodi zaidi ya nusu ya maambukizi yote barani Afrika.**

Mataifa mengi barani Afrika awali yaliweka mikakati kadhaa ya kuzuia kusambaa kwa maambukizi ya ugonjwa wa corona, ikiwamo kuwataka raia wake kusalia majumbani, kufunga mipaka yao pamoja na kufanya upimaji wa virusi hivyo.

Hata hivyo, athari kwa uchumi na hofu ya kutokea kwa baa la njaa vimesababisha nchi hizo kuanza kulegeza baadhi ya vikwazo hivyo kama zuio la kutotoka ndani.

Wataalamu wanasema janga la ugonjwa wa corona limeanza kusambaa kwa haraka barani humo.

Afrika Kusini, nchi yenye huduma bora zaidi za afya barani Afrika, awali ilionekana kufanikiwa katika kukabiliana na virusi vya corona.

Shirika la Habari la Reuters linaripoti kuwa kwa sasa mfumo wa afya wa nchi hiyo unaelekea kuzidiwa hasa kutokana na idadi kubwa ya visa vya corona, uhaba wa vitanda vya wagonjwa pamoja na wahudumu wa afya kukosa vifaa vya kutosha kujikinga dhidi ya virusi hivyo hatari.

Nako nchini India takribani wahudumu wa afya 900,000 Ijumaa walianza kushiriki mgomo wa siku mbili, wakilalamikia kile wanachosema ni kukosa vifaa vya kujikinga dhidi ya ugonjwa wa corona, ilhali wanafanya kazi katika mazingira hatari ya kuambukizwa.

Kwa mujibu wa mwandaalizi wa mgomo huo AR Sindhu wahudumu hao pia wanataka kuongezewa malipo.

Hayo yakijiri, idadi ya maambukizi nchini humo imepita milioni mbili, huku watu 41,000 wakifariki dunia kutokana na ugonjwa wa corona.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya nchini humo, katika muda wa saa 24 ziliopita, nchi hiyo imeripoti visa 62,538 vya maambukizi ya virusi vya corona na kufanya idadi ya watu walioambukizwa kufikia milioni mbili.

Kulingana na wizara hiyo pia, watu 886 wamekufa kutokana na ugonjwa wa corona na kufanya idadi ya vifo kupindukia 41,585. **DW**




Mmoja wa wakazi wa mji wa Nagasaki nchini Japan akiwa katika moja ya kaburi akiadhimisha kumbukumbu ya miaka 75 tangu mji huo uliposhambuliwa kwa bomu la nyuklia na Marekani. **PICHA: REUTERS**

## Vyombo vya habari vyagoma kulaani shambulizi

**BISSAU,** Guinea

VITUO vya radio nchini Guinea-Bissau vilisitisha matangazo kwa saa 24 Alhamisi kuonyesha mshikamano baada ya kituo kimoja cha Radio Capital FM kushambuliwa.

Naibu Mkurugenzi, Sabino Santos, alieleza kuwa Alfajiri Julai 26, kikundi cha watu waliokuwa wamevaa nguo za polisi na wakiwa wana silaha za kivita waliingia katika ofisi za Capital FM katika Mji Mkuu, Bissau.

Alisema vifaa vya kituo hicho ikiwamo kifaa cha kurushia matangazo, kuchanganya sauti na kompyuta viliharibiwa.

Tangu wakati huo kituo hicho kimekuwa kikitangaza habari na maudhui nyingine kupitia mtandao wa Facebook.

Vituo kadhaa binafsi vya radio katika mji huo mkuu na vituo 23 vya radio za kijamii kote katika nchi hiyo iliyoko Afrika Magharibi vilisitisha matangazo ya habari na programu nyingine.

"Tunataka tuonyeshe kwamba sekta ya habari ni muhimu kwa maendeleo ya nchi," alisema Diamantino Domingos Lopes, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyakazi na uongozi.

"Tumetaka tusitangaze siku moja kuonyesha kukerwa kwetu na kile kinachoendelea katika sekta hii," alisema Lopes.

Lopes alieleza shambulizi hilo dhidi ya Capital FM kuwa ni ukiukaji uliopindukia wa uhuru wa kujielezea.

Jumuiya hiyo ilikuwa imetaka mamlaka husika nchini Guinea-Bissau ifikapo Jumatano wawe wamejibu madai yao kwa wahusika kuwajibishwa na kufikishwa mahakamani.

Polisi wamewaambia waandishi kuwa wanaendelea na uchunguzi, ingawaje hakuna tamko rasmi lililotolewa hadi sasa na walioshambulia kituo hicho hawajaweza kutambuliwa.

Shambulizi katika kituo cha Capital FM lililaaniwa na maofisa wa serikali ya Guinea-Bissau ikiwamo kauli ya Waziri katika ofisi ya Rais, Mamadu Serifo Djaquite.

Pia washirika watano wa kimataifa wa nchi hiyo wamelaani shambulizi hilo ikiwamo: Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya nchi zinazoongea Kireno, Umoja wa Ulaya na Umoja wa Mataifa. **VOA**

# Rais Museveni kuwachukulia hatua wanajeshi

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni ametoa amri kwamba wanajeshi wa Rwanda wanaodaiwa kuingia nchini mwake na kuwateka nyara raia wachukuliwe hatua.

Rais wa Uganda, Museveni na mwenzake wa Rwanda, Paul Kagame wamekuwa katika mvutano wa kisiasa kwa muda mrefu, huku kila mmoja akimtuhumu mwenzake kutaka kumwangusha kiutawala.

Mvutano baina ya marais hao wawili uliwahi kusababisha kufungiana mipaka, huku kila mmoja akimnyooshea kidole mwenzake na kumtuhumu kuwa ndiyo chanzo cha kutofautiana.

Agizo la kuchukuliwa hatua kwa wanajeshi wa Rwanda lilielekezwa kwa wakuu wa wilaya zinazopakana na Rwanda kufuatia visa kadhaa vya raia wa Uganda kukamatwa na majeshi ya Rwanda wakiwa ndani ya mipaka ya Uganda.

Aidha, Rais Museveni aliwataka raia wa Uganda kutothubutu kuvuka mpaka kwenda Rwanda, akisema wanaweza kushukiwa kushiriki biashara za magendo.

Kulingana na taarifa ya ofisi ya Rais Uganda, utawala wa Rwanda umeamrisha watu wanaopatikana wakishiriki biashara ya magendo kwenye mipaka na Uganda wapigwe risasi.

Hivi majuzi, maiti ya raia wa Uganda aliyedaiwa kutekwa nyara ilikabidhiwa kwa viongozi wa wilaya na wakuu wa serikali ya Rwanda.

Maagizo mapya ya Rais Museveni yanazusha mashaka kuhusu ufanisi wa juhudi za upatanishi kati ya Rwanda na Uganda, unaozihusisha Angola na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. **DW**

# 'BALE ANAPOTEZA MUDA WAKE TU'




**MADRID,** Hispania

GARETH Bale "ana poteza muda wake" pale Bernabeu na mchezaji huyo na klabu lazima "wamalize hali hiyo" kipindi hiki cha majira ya joto, amesema Rais wa zamani wa Real Madrid, Ramon Calderon.

Mshambuliaji huyo wa Wales, Bale mwenye umri wa miaka 31, hakuwa sehemu ya kikosi cha Real Madrid kilichoondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Manchester City, Ijumaa, huku kocha Zinedine Zidane akisema mchezaji mwenyewe "hakutaka kucheza".

"Inahuzunisha. Kuona mchezaji kama yeye akiwa jukwaani," alisema Calderon kuhusu hali ngumu aliyokuwa nayo Bale msimu huu. "Nafikiri ujuzi na kipaji chake havijaisha, bado ni mchezaji mzuri ambaye anaweza kucheza kwa kiwango cha juu katika timu yoyote kubwa duniani.

"Kwa hiyo, nafikiri wanatakiwa kutafuta suluhisho la kumaliza jambo hili kwa faida ya pande zote mbili. "Kama hataki kupunguza mshahara wake, kitu ambaco kinaeleweka, watatakiwa kutafuta njia nyingine ya kumaliza hali hii."

Bale amebakiza miaka miwili katika mkataba wake na Real, ambao unamfanya alipwe mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki.

Ameanza katika mechi 14 kwenye mashindano yote msimu wa 2019-20, na amecheza mara mbili tu baada ya kurudi tena kwa msimu wa Ligi ya Hispania, Juni baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# Pirlo kocha mpya Juve

**TURIN,** Italia

JUVENTUS imemteua, Andrea Pirlo kama kocha wao mkuu mpya kwa mkataba wa miaka miwili.

Kiungo huyo wa zamia wa timu ya Taifa ya Italia, alichukua mikoba ya kuwa kocha wa timu ya Juve chini ya umri wa miaka 23 siku tisa tu na sasa amechaguliwa kumrithi, Maurizio Sarri.

Sarri alifukuzwa Jumamosi baada ya Juve kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora kwa faida ya bao la ugenini baada ya ushindi wa uwiano wa mabao 2-2 dhidi ya Lyon.

Awali mchezaji wa zamani wa Juve na sasa kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane pamoja na kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino na wa Lazio, Simone Inzaghi, walikuwa wakitajwa kupewa nafasi hiyo.

Pia kulikuwa na uvumi kwamba, kocha wa zamani wa timu ya Taifa ya Italia, Roberto Mancini angeweza kupewa nafasi hiyo, lakini klabu hiyo imeamua kumpandisha Pirlo.

"Kuanzia leo atakuwa kocha wa Juventus, ni sehemu ya maamuzi ya klabu na kwamba tunamuamini baada ya kuwa kiongozi katika kikosi chetu cha kwanza, na baada ya kumchagua kuwa kocha wa Juventus chini ya umri wa miaka 23," ilisomeka taarifa ya klabu hiyo.

"Maamuzi ya leo yameegemea zaidi kutokana na imani yetu kwa Pirlo kwa kile alichokionyesha wakati akianza kuwa kwenye benchi letu la ukocha, na tumeshawishika awe kocha wetu mpya."

Pirlo aliondoka Juve mwaka 2015 baada ya 'Bianconeri' hao waliokuwa wanawania kutwaa mataji matatu, kufungwa 3-1 kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Barcelona.

Alitumia miaka miwili kucheza kwenye Ligi Kuu ya Marekani (MLS), akiwa na klabu ya New York City, kabla ya kustaafu kucheza soka.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2006 na Italia, ni bingwa mara sita wa Serie A, akiwa ameshinda mara mbili na Milan na mara nne na Juve. Alishinda taji la Ligi ya Mabingwa mara mbili akiwa mchezaji wa Milan mwaka 2003 na 2007.





# Setien achambua ushindi Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Quique Setien, anafikiri walitawala vizuri kwenye mchezo wao wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya timu 16-bora dhidi ya Napoli - ingawa alikuwa na woga kwenye benchi lake.

Mabao kutoka kwa Clement Lenglet, Lionel Messi na Luis Suarez yakawawezesha kushinda 3-1 pale katika dimba la Camp Nou, Jumamosi na hivyo kusonga mbele kwa ushindi wa uwiano wa mabao 4-2.

Barca walikuwa wanaongoza kwa mabao 3-0 na bao jingine la Messi lilikataliwa kwa madai ya kuunawa mpira kipindi cha kwanza, na ingawa Lorenzo Insigne alifunga kwa mkwaju wa penalti, lakini hakuweza kuisaidia Napoli kupata ushindi.

Barca ilimaliza ndoto mbaya za kutolewa na Liverpool na AS Roma kwenye mchezo wa pili wa hatua ya mtoano misimu miwili iliyopita, hivyo Setien aliridhishwa na kiwango cha timu yake ilichoonyesha dhidi ya Napoli, ingawa hofu ilimtawala.

"Ilikuwa ni kile tulichokuwa tunakitaka, kuchukua ushindi mwanzo na kujiweka kwenye nafazi nzuri ya kucheza bila presha kubwa kipindi chote cha mchezo kilichobaki," alisema akiiambia Movistar.

"Tulikuwa kwenye kiwango kizuri na tulistahili ushindi. "Ni kweli walianza kwa presha kubwa dakika za mwanzo. Kwa uhakika Napoli ni timu nzuri si rahisi kufanya kile tulichofanya. Ni moja ya timu bora Italia.

"Tulitawala mchezo vizuri, tulikuwa na kipindi kizuri cha kwanza, na cha pili waliongeza nguvu, lakini hawakuleta hatari nyingi kwetu.

"Bao la pili lingewapa morali kubwa na kutuweka kwenye hatari. Ni kawaida kuwa na hofu, bila shaka yoyote nilikuwa muoga nilipokuwa kwenye benchi langu."

## HABARI MICHEZO

# Suarez: Mchezo dhidi ya Bayern utakuwa 50-50

**BARCELONA,** Hispania

BAYERN Munich wana nafasi kubwa kwenye taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini Luis Suarez amesema mchezo wa robo fainali dhidi ya Barcelona utakuwa 50-50.

Barca waliibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Napoli 3-1 pale kwenye dimba la Camp Nou Jumamosi na kupata ushindi wa uwiano wa mabao 4-2, na sasa wataikabili Bayern Ijumaa kwenye Uwanja wa Estadio da Luz, ambao waliifunga Chelsea 4-1 na kusonga mbele kwa ushindi wa uwiano wa 7-1.

Na Suarez sasa anaona kwamba mchezo huo hautakuwa rahisi na kwamba wanatakiwa kupambana na kuimarisha kiwango chao.

"Kila mmoja ana nafasi kwenye mchezo huu mmoja, ni 50-50," alisema Suarez akiiambia Movistar.

"Bayern ni wapinzani wakubwa, wao wana nafasi kubwa kweye mbio za kuliwania taji hili, kama ilivyo timu zote nane mjini Lisobon, lakini 11 dhidi ya 11 kwa dakika 90.

"Unatakiwa kucheza mchezo ambao unaona kabisa unacheza kwa kiwango cha kuvutia ili kufuzu nusu fainali."

Katika mchezo dhidi ya Napoli: "Tulifanya kile tulichotakiwa kufanya. Kwa wiki mbili tangu kumalizika kwa LaLiga tumekuwa tukijiandaa kwa ajili ya mchezo huu, huku tukijua kwamba utakuwa mgumu," alisema katika mahojiano hayo.

"Ni jambo muhimu kwamba tumefuzu kucheza robo fainali na sasa tunafikiria kuhusu mpinzani wetu anayefuata."






# KICHAPO CHA BAYERN FUNZO KWETU - LAMPARD

**MUNICH,** Ujerumani

FRANK Lampard ameahidi Chelsea watapata uzoefu kutokana na kipigo kikubwa walichokipata kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora kutoka kwa Bayern Munich na watarudi wakiwa imara zaidi msimu ujao.

Chelsea walichapwa mabao 4-1 na Bayern kwenye mchezo wa pili juzi Jumamosi katika dimba la Allianz Arena, hivyo kutolewa kwa uwiano wa mabao 7-1.

Robert Lewandowski alifunga mara mbili, na kutoa pasi za mwisho mbili kwa mabao ya Ivan Perisic na Corentin Tolisso, huku Tammy Abraham akifunga la kufutia machozi.

Baada ya matokeo hayo, Lampard alisema watatumia kipigo hicho kutoka kwa Bayern kama sehemu ya kujifunza yeye pamoja na wachezaji wake.

"Ulikuwa uzoefu mzuri kwa upande wetu dhidi ya Bayern na uzoefu wao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwani wachezaji wetu wengi walikuwa ndio msimu wao wa kwanza," alisema akiiambia BT Sport.

"Naweza kuona wapi ambapo tunataka sisi kwenda na najua tutarudi tena kwenye mashindano haya.

"Walicheza kwa kiwango cha kuvutia zaidi. Ni ngumu kuzungumza baada ya kichapo cha 4-1, na sina furaha, lakini kama tungefunga mabao mawili pengine tungekuwa na kitu fulani."

# *Zidane apuuza uvumi kutimuliwa Real Madrid*

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane ameibuka na kupuuza uvumi kuhusu majaliwa yake, akisisitiza kwamba ataendelea kuwa kocha wa Real Madrid msimu ujao.

Hatimaye msimu wa Madrid wa 2019-20 ulifikia mwisho katika Uwanja wa Etihad baada ya kuchezea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Manchester City kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na hivyo kuondolewa kwa uwiano wa 4-2.

Klabu ina Kombe la Ligi ambalo ililitwaa msimu huu ikiwa ni mara ya kwanza tangu mwaka 2017.

Alipoulizwa kama mipango yake ni kuendelea kuwa kocha hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu kwa msimu ujao wa 2020-21, Zidane alijibu kwa ghadhabu.

"Nido, mimi si nipo hapa, mimi ni kocha wa Madrid hadi kitu kingine kitokee ambacho kipo nje ya uwezo wangu. Mimi nipo hapa bila shaka yoyote," alisema.

"Hutakiwa kufikiria kilichotokea. Mimi ni kocha wa Madrid, ndio hivyo.

"Hakuna maswali zaidi ya kuuliza kuhusu hili. Sasa tunakwenda kupumzika na tutatudi kwa ajili ya msimu mpya."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI APUUZIA REKODI, AIFIKIRIA BARCA

●●● Tuna mchezo mwingine wa mtoano na tunatakiwa kucheza vizuri kama...

**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski amesema hafikirii tuzo binafsi kwa rekodi ya mabao, kwani yeye akili yake ni kuhakikisha anaisaidia Bayern Munich kuifunga Barcelona kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kama alivyofunga mawili dhidi ya Chelsea, Jumamosi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland amejiimarisha zaidi msimu huu kwa kufikisha mabao 53 katika mashindano yote wakati akifunga mara mbili na kutoa pasi za mwisho mbili, kwenye ushindi wa 4-1 pale kwenye dimba la Allianz Arena na kushuhudia Bayern ikifuzu robo fainali kwa ushindi wa uwiano wa mabao 7-1.

Lewandowski sasa amefikisha mabao 13 katika mechi saba za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, akipitwa manne na Cristiano Ronaldo wakati alipoweka rekodi ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja wa 2013-14.

**Lakini straika huyo mwenye umri wa miaka 31, alisisitiza hafikirii kuhusu rekodi binafsi, kwani nia yake ni kuisaidia timu kushinda kwenye robo fainali Ijumaa ijayo mjini Lisbon, ambapo Barca inawasubiri baada ya ushindi wao wa uwiano wa mabao 4-2 dhidi ya Napoli.**

"Sifikiri hilo," alisema Lewandowski akiambia Sky Sport Germany wakati alipoulizwa kuhusu rekodi ya Ronaldo. "Tuna mchezo mwingine wa mtoano na tunatakiwa kucheza vizuri kama timu.

"Kitu cha muhimu ni kucheza vizuri na kutinga hatua inayofuata. Tunatakiwa kuonyesha kama timu kwamba sisi ni bora (kuliko Barcelona) ili kufuzu nusu fainali.

"Barcelona mara zote ni hatari na wacheza soka la kuvutia. Tunatakiwa kuwa kwenye kiwango chetu kuanzia dakika ya kwanza na kuonyesha ubora wetu. Timu bora itacheza hatua inayofuata."

Lewandowski alihusika katika kila bao kwa Bayern katika ushindi huo wa uwiano wa mabao 7-1 dhidi ya Chelsea, akiwa pia alifunga mabao na kutengeneza moja kwa Serge Gnabry katika mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa timu 16-bora pale Stamford Bridge.

Kocha Mkuu, Hansi Flick alikisifia kikosi chake chote si tu Lewandowski, ambaye amefunga mabao mengi zaidi kwa msimu wa 2019-20 kuliko mchezaji yeyote kwenye ligi tano kubwa za Ulaya.

"Alifunga mara mbili, hivyo naweza kusema kila mchezo lazima afunge," alisema bosi huyo wa Bayern.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUMUUZA LACAZETTE

ARSENAL itamuuza mshambuliaji wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 29, kwa Atletico Madrid kwa pauni milioni 30 haraka tu baada ya Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 31 raia wa Gabon atakaposaini mkataba mpya. ***(Star Sunday)***

### CHELSEA YAONYWA KWA KAI

MKURUGENZI wa soka wa Bayer Leverkusen, Rudi Voller ameionya Chelsea kwamba klabu yake haitakubali kiasi chochote zaidi ya pauni milioni 90 wanazozitaka kwa ajili ya kumuuza kiungo wa Ujerumani, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### YAMCHELEWESHA COUTINHO

KIUNGO wa Barcelona na Brazil, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 28, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo kule Bayern Munich, hatafanya maamuzi yoyote kuhusu majaliwa yake hadi baada ya kumalizika kwa michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sport)***

### BRIGHTON WAMZUIA BEN

KLABU ya Brighton imekataa ofa ya pauni milioni 22 kutoka kwa Leeds waliopanda Ligi Kuu kwa ajili ya mlinzi wao wa kati, Ben White mwenye umri wa miaka 22, ambaye alitumia msimu mmoja akicheza kwa mkopo kule kwenye dimba la Elland Road. ***(Sky Sports)***

### CHELSEA YAMTAKA STONES

CHELSEA inamwangalia mlinzi wa Manchester City, John Stones na wana matumaini ya kumsajili nyota huyo wa timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 26 kwa pauni milioni 20. ***(Sunday Mirror)***

### ARSENAL KWA SANSON

ARSENAL imeingia kwenye mbio moja za kuwania kumsajili kiungo wa Marseille, Morgan Sanson, huku Tottenham na West Ham pia zikionyesha nia ya kumtaka raia huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 25. ***(Le10 Sport, via Sunday Express)***

### WALKER-PETERS KUSEPA SPURS

MLINZI wa Uingereza, Kyle Walker-Peters mwenye umri wa miaka 23, yupo kwenye hatua ya mwisho kuondoka Tottenham kwa pauni milioni 12 baada ya kufikia makubaliano binafsi na Southampton, ambako alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita akicheza kwa mkopo. ***(Sunday Mirror)***

### KIPA MPYA ASAKWA ARSENAL

ARSENAL imeripotiwa kwamba inatafuta golikipa mpya kwa ajili ya kumsaidia Emiliano Martinez, wakati wakiwa hawana uhakika kipa wao chaguo la kwanza, Bernd Leno atakaa nje kwa muda gani baada ya kuumia goti. ***(Sun on Sunday)***

### KOSTAS AGOMBEWA EPL

LEICESTER na Liverpool zinawania kumsajili mlinzi wa kushoto wa Olympiakos na Ugiriki, Kostas Tsimikas mwenye umri wa miaka 24, ambaye gharama yake inaweza kuwa pauni milioni 12. ***(Mail on Sunday)***

### DORTMUND KUMFUNGA SANCHO

BORUSSIA Dortmund itatoa ofa kwa winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, ili asaini mkataba mpya, kama Manchester United hawataweza kufikia bei ya pauni milioni 100 wanazotaka ili kumwachia, ikiwa mwisho wake ni leo. ***(Bild - in German)***

HABARI MICHEZO

## Simba Kings yaanza vema Ligi ya Kriketi

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya mchezo wa Kriketi ya Simba Kings, imeanza vema ligi ya mchezo huo (APL) baada ya kuishinda Buffalo Blasters kwa wiketi tatu katika mechi iliyopigwa jijini Dar es Salaam Jumamosi iliyopita.

Ligi hiyo, ambayo hufanyika kila mwaka, inaandaliwa na Chama cha Mchezo wa Kriketi nchini (TCA) ikiwa na lengo la kuuendeleza mchezo huo. Buffalo Blasters ilipata fursa ya kuanza kupiga mpira na kufunga mikimbio 121 huku ikipoteza wiketi sita.

Salum Jumbe alipata mikimbio 37 na hivyo alikuwa mpigaji aliyepata mikimbio mingi zaidi katika timu hiyo, akifuatiwa na Ankit Baghel aliyepata mikimbio 27. Yakesh Patel alipata mikimbio 15, Goodluck Andrew alipata mikimbio 14 wakati Mohamed Omary alimaliza na mikimbio 10.

Mohammad Ali wa Simba Kings alimaliza na wiketi mbili wakati wa fursa ya timu yake kurusha mpira, huku wachezaji wengine, nahodha Zafar Khan, Benson Mwita na Jatin Prajapati, wakipata wiketi moja kila mmoja.

Simba Kings walifanikiwa kupata idadi ya mikimbio iliyotakiwa ili waweze kushinda, ambayo ni 122, wakati wa zamu yao ya kupiga mpira, huku wakipoteza wiketi saba, na kuibuka na ushindi.

## Mlandege yapewa kombe lao Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF) limekabidhi Kombe la Ubingwa wa Ligi Kuu na mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 kwa bingwa wa ligi hiyo msimu wa 2019/20, timu ya Mlandege FC.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo iliyofanyika juzi katika Uwanja wa Mau, baada ya kumalizika mchezo maalum kati ya mabingwa hao dhidi ya timu ya Taifa ya Vijana ya Zanzibar chini ya umri wa miaka 20 na Malandege kushinda bao 1-0, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud.

ZFF pia ilitoa zawadi katika vipengele sita ambavyo ni Mchezaji Bora wa msimu kutoka Mafunzo FC, Ahmed Maulid Omar aliyezawadiwa viatu vya kuchezea mpira pamoja na pesa taslimu, na mchezaji bora chipukizi kutoka Mlandege, Masoud Rashid Juma aliyezawadiwa pesa taslimu pamoja na viatu vya soka.

# VODACOM YAAHIDI NEEMA KUENDELEZA LIGI KUU BARA

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU ikipongezwa kwa jitihada zao za kuendeleza soka nchini, Kampuni ya Kidigitali na Teknolojia ya Mawasiliano ya simu inayoongoza Tanzania na Mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu, Vodacom imeahidi kuendelea kuwa mdhamini wa ligi hiyo.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam Ijumaa iliyopita katika hafla ya utoaji tuzo kwa washindi wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara kwa msimu wa 2019/20, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, aliipongeza Kampuni ya Vodacom kwa jitihada zao za kusaidia maendeleo ya mpira wa miguu Tanzania kwa miaka mingi.**

"Udhamini wa Ligi Kuu ya Taifa unaotekelezwa na Kampuni ya Vodacom Tanzania umeweza kukuza vipaji na medani ya mpira nchini, wito wangu kwa wadhamini wa mpira ni kuwekeza katika ngazi za kati na chini ili kuinua mpira kuanzia ngazi za chini," alisema Jafo.

Naye Mkurugenzi wa Kitengo cha Masuala ya Biashara wa Vodacom Tanzania, Linda Riwa, aliwapongeza washindi wote kutoka katika makundi mbalimbali na kuwahakikishia kwamba kampuni hiyo itaendelea kusaidia kukuza kiwango cha mpira wa miguu Tanzania.

"Kama mnavyofahamu kwamba kampuni ya Vodacom Tanzania imeingia mkataba na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), ambapo TFF watapokea kiasi cha Sh. bilioni tisa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2019 - 2020.

"Tutaendelea kusaidia maendeleo ya mpira wa miguu Tanzania kwa kulea vipaji na kukuza sekta nzima ya mpira wa miguu jambo ambalo litanufaisha klabu za mpira wa miguu, wachezaji, marefa, washika vibendera, makocha, wasambazaji, makandarasi na kutoa ajira.

"Ninawahakikishia tena utayari wa Kampuni ya Vodacom Tanzania katika kusaidia maendeleo ya mpira wa miguu na sekta nzima inayozungukia mpira wa miguu Tanzania kwa kudhamini Ligi Kuu. Pia tunatazamia kushuhudia msimu bora zaidi wa Ligi Kuu katika siku zijazo," alihitimisha Linda.

Rais wa TFF, Wallace Karia alisema: "Kiwango cha mpira wa miguu nchini kimekua kufikia kiwango kinachoshuhudiwa sasa ambapo wachezaji wengi wa timu ya taifa wanacheza katika klabu mbalimbali za kimataifa, jambo hili linadhihirisha juhudi za wapenzi wa mpira na wadau wa mpira wa miguu kama vile Kampuni ya Vodacom Tanzania ambao wamefanikisha."

Mchezaji Bora na Kiungo Bora wa mwaka, Clatous Chama kutoka Klabu ya Simba, yeye alieleza kufurahia kuchaguliwa kuwa miongoni mwa wachezaji bora wa mpira wa miguu nchini katika kutoa wito kwa mashirika mengine kusaidia katika kukuza soka nchini.

"Nimefurahi kuchaguliwa miongoni mwa wachezaji bora wa msimu huu. Ninawashukuru wadau wote wa mpira wa miguu ikiwamo Vodacom Tanzania ambao wanasaidia mpira wa miguu Tanzania na kuchangia katika kukuza viwango na vipaji vya wachezaji chipukizi."

Tuzo ya timu bora ilinyakuliwa na Simba, kocha bora wa msimu ilikwenda kwa Sven Vandenbroeck wa Simba, beki bora ilikwenda kwa Nico Wadada (Azam FC). Patson Shikala wa Mbeya City alishinda goli bora, tuzo ya mchezaji bora chipukizi ilikwenda kwa Novatus Dismas wa Biashara United FC na tuzo ya kipa bora ilinyakuliwa na Aishi Manula wa Simba.

Tuzo ya timu yenye nidhamu ilichukuliwa na Kagera Sugar FC wakati tuzo ya mwamuzi bora ilichukuliwa na Ramadhan Kayoko wa Dar es Salaam na tuzo ya mwamuzi bora msaidizi ilichukuliwa na Frank Komba wa Dar es Salaam na mwisho Tuzo ya Mafanikio kwenye Maisha (Lifetime Achievement) ilikwenda kwa mchezaji wa zamani wa Klabu ya Pan African, Yanga na timu ya Taifa, Sunday Manara. Jumla ya thamani za tuzo hizo ni zaidi ya Sh. milioni 263.



Kikosi cha Rifa FC, kilichowatupa nje mabingwa watetezi Kirengo FC kwa kuwachapa mabao 4-0 kwenye mechi ya robo fainali ya Umoja Cup iliyopigwa mwishoni mwa wiki kwenye Uwanja wa Maji Sota, Rorya. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Umoja Cup sasa yafikia nusu fainali Rorya

**Na Mwandishi Wetu,** RORYA

MICHUANO ya Kombe la Umoja (Umoja Cup) imefikia patamu ambapo kesho Maji FC itashuka dimbani kumenyana na Town Stars katika mechi ya nusu fainali ya kwanza itakayopigwa kwenye Uwanja wa Maji Sota, Shirati wilayani Rorya.

Hata hivyo, mchuano mkali zaidi unatarajiwa kuwa keshokutwa, Jumatano, wakati Rifa FC iliyomtoa bingwa mtetezi wa michuano hiyo, Kirengo FC kwa kuichapa mabao 4-0 kwenye mechi ya robo fainali, itakaposhuka dimbani kuvaana na Bumbombi katika uwanja huo.

Akizungumza na mwandishi wetu jijini Dar es Salaam jana, mwandaaji wa michuano hiyo, Peter Owino, alisema michuano ya msimu huu imekuwa na ushindani mkubwa pamoja na msisimko kutoka kwa mashabiki.

"Huu ni mwaka wa nane ninaandaa mashindano haya na yamekuwa yakifanyika kila mwaka, lakini mwaka huu yamekuwa na ushindani mkubwa huku yakizidi kuwavutia mashabiki wengi kuhudhuria uwanjani kushuhudia.

"Tangu michuano ya mwaka huu imeanza Julai Mosi, ikichezwa kwa mtindo wa ligi na kushirikisha timu 20 zikiwa katika makundi manne hadi inafikia hatua ya nusu fainali, ushindani umekuwa mkubwa sana, tofauti na miaka mingine," alisema Owino.

Alisema mbali na mashindano hayo kuwa burudani kwa wakazi wa Rorya, lakini lengo kubwa ni kuibua vipaji na kuikutanisha jamii pamoja ili kujenga amani na ushirikiano katika masuala mbalimbali.

"Lakini mashindano haya ndiyo yanayotoa wachezaji kwenda kuunda timu ya Maji inayoshiriki Ligi ya Mkoa," alisema.

Owino alisema fainali ya michuano hiyo itapigwa Jumapili wiki katika Uwanja wa Maji Sota huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Ofisa Michezo wa Wilaya ya Rorya.

Kuhusu zawadi kwa mshindi, Owino alisema mbali na kombe bingwa wa michuano hiyo ataibuka na fedha taslimu kiasi cha Sh. 300,000 huku mshindi wa pili akijinyakulia Sh. 200,000 na watatu Sh. 100,000.

# Michezo

Jumatatu Agosti 10, 2020

Nipashe




Lewandowski apuuzia rekodi UKURASA 22

NIMEACHIA NGAZI...



Senzo Mbatha Mazingisa, ambaye jana alitangaza kujiuzulu nafasi yake ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba. **PICHA: MAKTABA**

## Yanga yazidi kuimarisha ukuta wake

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU ikiwa imeshatangaza kuachana rasmi na mabeki wake wawili, beki wa kati, Kelvin Yondani na wa pembeni Juma Abdul, Yanga imezidi kuimarisha ukuta wake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Bara baada ya jana kumsajili beki Kibwana Ally Shomari kutoka Mtibwa Sugar ya Morogoro.

Tayari Yanga ilishawasajili mabeki watatu; beki wa kati, Abdallah Haji Shaibu 'Ninja', ambaye alisaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia, klabu hiyo ikiwa ni mara yake ya pili kurejea kuichezea klabu hiyo.

Mabeki wengine waliosajiliwa msimu huu ni beki wa kati, Bakari Mwamnyeto akitokea Coastal Union na Yasin Mustapha kutoka Polisi Tanzania ambao watasaidiana na Lamine Moro na Said Makapu waliobakishwa kutoka kikosi cha msimu uliopita.

Mbali na mabeki hao, wachezaji wengine waliosajili na Yanga dirisha hili linalotarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwezi huu ni pamoja na kiungo Zawadi Mauya kutoka Kagera Sugar na mshambuliaji Wazir Junior kutoka Mbao FC.

Ally Shomari alisaini mkataba wa miaka miwili jana tayari kuanza kutumikia timu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam.

# Mo afunguka Senzo kujiuzulu

## Asema Simba ni kubwa kuliko mtu binafsi, Morrison, Yanga watajwa kuwa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI akiwa ameanza kwa mafanikio huku akiipeleka Klabu ya Simba kuendeshwa kisasa zaidi, Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mbatha Mazingisa ametangaza kujiuzulu nafasi yake hiyo kuanzia jana.

**Katika taarifa yake fupi aliyoiposti jana kupitia akaunti yake ya instagramu, Senzo ameishukuru klabu hiyo kwa mafanikio yaliyopatikana kwenye kipindi kifupi akiiongoza klabu hiyo kama Ofisa Mtendaji Mkuu.**

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohammed "Mo" Dewji, jana aliwatuliza mashabiki na wanachama wa klabu hiyo akiwataka kutulia kila kitu kitakwenda vizuri.

"Tumetoka mbali na bado safari inaendelea; tumepita mengi Wanasimba wenzangu. Nawaomba Wanasimba wote mtulie, Simba SC ni kubwa kuliko mtu mmoja. Sisi viongozi tunawatumikia usiku na mchana bila kujali maslahi ya mtu binafsi bali Simba. Kazi inaendelea, tuko imara," alieleza Mo.

Katika msimu wa 2019/20 uliomalizika, akiwa mtendaji mkuu Senzo ameiongoza Simba kutwaa mataji matatu ambayo ni pamoja na Ngao ya Jamii, Ligi Kuu Bara na Kombe la Shirikisho, FA Cup huku akiwa mstari wa mbele kuhakikisha nidhamu inazingatiwa na kila mchezaji klabuni.

Hata hivyo, taarifa kutoka vyanzo mbalimbali jana zilidai kudai kuwa kujiuzulu kwa Senzo kumetokana na kutokuwa na maelewano mazuri ndani ya Simba kwenye masuala ya uongozi kwa kuingiliwa majukumu yake ikiwamo usajili wa kiungo mshambuliaji, Mghana Bernard Morrison.

"Unajua Senzo, hataki uswahili, yeye anataka kila kitu kiendeshwe kwa kufuata taratibu na kila mmoja kuhusika vema katika nafasi yake bila kuingiliwa, baadhi ya mambo bado viongozi wa Simba wamekuwa wakimwingilia ama kufanya bila kumshirikisha wakati ndiye mtendaji mkuu," kilieleza chanzo kimoja jijini Dar es Salaam jana na kuongeza.

"Suala la usajili wa Morrison nalo linaelezwa ni moja ya mambo ambayo yamemkera kwani hakufahamu kinachoendelea kuhusu mchezaji huyo hadi alipotangazwa, kitu ambacho anaona si sahihi akiwa kama mtendaji mkuu wa klabu."

Pamoja na Senzo kutokuweka wazi sababu za kujiuzulu, lakini taarifa zingine zilidai kuwa alisaini mkataba wa mwaka mmoja ambao kimsingi unamalizika mwezi ujao, hivyo ameamua kutoendelea ili kumulika kwingineko, huku baadhi wakimhusisha na kuhamia upande wa pili, Yanga.

Pamoja na mambo mengi mazuri na ya kimkakati wa mafanikio aliyofanya, lakini usajili wake makini wa kiungo Luis Miquissone, ni moja ya alama muhimu ya kujivunia kwa mashabiki wa klabu hiyo aliyowaacha.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002